epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumatatu Novemba 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581850
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
MWANGA WA JAMII
www.instagram.com/theguardian_newspaper

UCHAGUZI UJAO

## Lissu aweka msimamo upinzani kuungana

UKURASA 2



Rais mstaafu Jakaya Kikwete (wa pili kushoto) akimkabidhi tuzo na cheti cha shukurani kwa mchango, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa pili kulia) baada ya NMB kukabidhi hundi ya Sh. bilioni moja kusaidia matibabu ya watoto katika taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu na kushoto ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Suleiman Jaffo. **HABARI KAMILI UKURASA 4**

UKURASA WA 2
**ACT** kutinga ofisini kwa waziri kushtaki wasimamizi kufunga ofisi, kutowapa fomu wagombea upinzani

UKURASA WA 9
**Serikali** yashtukia usafirishaji mabinti kutumikishwa kingono

UKURASA WA 19
**Bosi** wa Dar24 afunguka siri ya kupotea kwake

## Utafiti wabaini wanaoishi na VVU hatarini zaidi magonjwa ya akili

UKURASA 7

## Kiboko auawa kwa risasi, wananchi wapata kitoweo

UKURASA 7



Wananchi wakifurahia kumwona kiboko aliyekuwa anakula mazao yao katika kijiji cha Ilungu, wilayani Magu jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Nipashe WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

MICHEZO GAMONDI AUKUBALI MUZIKI WA AZAM FC UK.24
KATUNI UK.6

# Mkenda: Tasnia ya habari iko hatarini kwa makanjanja

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Elimu, Sanyansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda, ametahadharisha kuwa kuna hatari kubwa teknolojia ikawaleta makanjanja wengi kwenye tasnia ya habari ambao hawana elimu na masuala ya habari kama hatua hazitachukuliwa haraka.

Amesema makanjanja hao wataonekana wao ndio wasemaji wa habari za propaganda ambazo zitawatenganisha waandishi wa habari na serikali na kusababisha mafarakano, wataondoa mshikamano kwa nchi na hivyo tasnia ya habari kupoteza nia kama mhimili wa nne usio rasmi.

Prof. Mkenda alisema hayo juzi wakati wa mkutano mkuu wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) unaofanyika mjini Singida na kuwashirikisha wenyeviti, makatibu na waweka hazina kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

"Teknolojia ya sasa hivi inasababisha habari tunazozipata hazitoki tu kwenye media (vyombo vya habari) ambazo tumezizoea, wapo watu wanajikalia wanaanzisha utangazaji na kuanza kusambaza habari, hawa nao wana nguvu ya kujenga au kubomoa.

"Kama Wizara ya Elimu tungepata mawazo yenu, tunaendelea kuelimishana waandishi wa habari kwa namna gani, mambo yapi mapya tuyaingize kwenye mitaala yetu, ni nini tufanye hata baada ya mtu kuhitimu kwa ajili ya kuendelea kujengeana uwezo," alisema.

Rais wa UTPC, Deogratius Nsokolo, alizitaka klabu za waandishi wa habari nchini kufanya kazi kwa kuzingatia mpango mkakati wa 2023-2025 unaotekelezwa na UTPC ili kuendelea kuwavutia wafadhili kusaidia taasisi hiyo badala ya kuendekeza migogoro.

Mkurugenzi wa UTPC, Kenneth Simbaya, alisema klabu zinatakiwa kutimiza wajibu kwa kuwa zisipofanya hivyo, UTPC itaonekana kuwa kikwazo cha yale ambayo yangeweza kupatikana kupitia umoja huo.

# Lissu aweka msimamo upinzani kuungana 2025

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Tanzania Bara, Tundu Lissu amesema mpango wa vyama vya upinzani kushirikiana katika baadhi ya maeneo wakati wa uchaguzi kwa ajili ya kuweka nguvu zaidi ya ushindi ni jambo jema.

Hata hivyo, mtaalamu huyo wa sheria amesema tatizo kubwa linalochangia jambo hilo lisiwezekane ni kwamba vyama vyenye uwezo wa kuweka wagombea havifiki hata vinne.

Lissu amesema jana kuwa vyama vingi vya upinzani nchini havina uwezo wa kusimamisha wagombea au kufanya kampeni na kwamba hata takwimu katika uchaguzi uliopita zinaonesha havifikishi asilimia tano ya kura za wabunge na asilimia tatu ya kura za Rais huku vyama vinavyofanikiwa kusimamisha wagombea maeneo mengi ya nchi vikionekana ni viwili tu -- Chama Cha Mapinduzi (CCM) na CHADEMA.

Ni kauli aliyoitoa mwishoni mwa wiki wakati wa mahojiano kwenye kipindi cha Medani za Siasa kinachorushwa na Star Tv.

"Tuzungumze ukweli; maeneo ya kuunganisha nguvu ni machache sana, sehemu kubwa ya vyama katika nchi hii, ni CCM na CHADEMA. Sasa huko ambako viko vyama hivyo viwili ukisema tuunganishe, tunaunganisha nguvu na nani ambaye hatumwoni kabisa? Hawapo kabisa hata kwenye mikutano, hawapo kwenye uchaguzi... tuunganishe nguvu kwa sifuri, ukijumlisha sifuri sawa na sifuri. "Kama vyama vya upinzani vipo na vimejipanga kuangalia maeneo ya kuunganisha nguvu kwenye chaguzi si jambo baya, tatizo ni kwamba vyama vya upinzani vyenye uwezo wa kuweka wagombea kwenye uchaguzi wowote ule katika nchi yetu ni vingapi hasa?" Lissu alihoji.

Alisema vyama vya siasa vilivyoandikishwa vipo zaidi ya 20, lakini ambavyo huwa vinaweka wagombea havifiki vinne.

"Una uhakikia CCM itaweka wagombea? Una uhakika CHADEMA itaweka wagombea kila mahali? Utakuwa na uhakika kwamba ACT-Wazalendo itaweka wagombea wote wanaohusika Zanzibar lakini baada ya hapo vyama vingine viko wapi?

"Ukitaka kujua nani ni nani katika uchaguzi wa Tanzania, angalia takwimu zozote za uchaguzi wetu. Pamoja na matatizo yote ya uchaguzi wetu, angalia takwimu za huo uchaguzi. Hivyo vyama vingine vyote, 2020 ukiondoa CCM na CHADEMA, havikufikisha asilimia tano ya kura za wabunge, havikufikisha asilimia tatu ya kura za Rais.

"Haviweki wagombea, havifanyi kampeni, vyama vingine hivi vinaishi katika madaftari ya Jaji Fransis Mtungi tu (Msajili wa Vyama vya Siasa nchini).

"Huko utavikuta lakini ukija huku waliko wananchi unakutana na viwili, vitatu, ukienda mikoani ni viwili, vitatu... ukienda kwa msajili wanakuambia aah... tuna vyama 23. Tuna tofauti ya vyama vilivyopo katika madaftari ya Jaji Mtungi na vyama ambavyo viko mtaani na vijijini katika nchi yetu," alisema Lissu.

Mwanasiasa huyo pia alitoa maoni yake kuhusu kuondolewa kwa Rigathi Gachagua katika kiti cha Naibu Rais wa Kenya, akisema hilo limetokana na mfumo wa uchaguzi na kikatiba wa nchi hiyo ambao Tanzania ina jambo la kujifunza kwake.

"Kwangu mimi ule utaratibu wa kumwondoa madarakani Naibu Rais wa Kenya, unathibitisha ushindi wa demokrasia ya nchi hiyo, unathibitisha ushindi wa mfumo wa kikatiba wa nchi hiyo ambayo imeweka utaratibu wa kumwondoa Makamu wa Rais madarakani na Rais mwenyewe kama ikionekana kwamba amefanya vitendo vinavyopingana au kukiuka katiba ya nchi yao.

"Wanachofanya Wakenya wanathibitisha ukuu wa katiba na misingi yake imara na misingi imara ya taasisi zao za dola pamoja na mambo makubwa kama hayo yanafanyika hadharani, bungeni waziwazi, mbele ya wananchi na uamuzi unafanywa na vyombo vyenye mamlaka ya kuamua kwa njia

UCHAGUZI WA MITAA

# ACT kutinga ofisini kwa waziri wasimamizi kutofungua ofisi

**Na Elizabeth Zaya**




Kiongozi wa ACT Wazalendo, Doroth Semu **PICHA:MTANDAO**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema kinapanga kumwandikia msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa orodha ya wagombea wote wa chama hicho walioshindwa kuchukua na kurejesha fomu kutokana na wasimamizi wa uchaguzi kutofungua ofisi.

Chama hicho kimedai kwamba baadhi ya wagombea wake walishindwa kurejesha fomu kutokana na kufanyiwa hujuma na baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi huo kufunga ofisi licha ya kuwa ndani ya muda.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Kiongozi wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu, Kamati ya Uongozi Taifa ya chama chake, imetoa maelekezo kwa Ofisi ya Katibu Mkuu wa chama hicho kuandika barua hiyo.

Alisema lengo la kuandika barua hiyo ni kutaka wagombea wote walioshindwa kurejesha fomu kwa sababu ya ofisi za wasimamizi wa uchaguzi kufungwa, warejeshwe kwenye orodha ya wagombea.

Pia alisema maelekezo mengine ya kamati ya kwa Katibu Mkuu wa Chama ni kutaka awasiliane na vyama vingine makini vya siasa na wadau wa demokrasia nchini, ili kuandaa kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha umma kupiga kura ya "hapana" kwa wagombea wote wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambao wamebaki peke yao au watabakishwa peke yao katika maeneo yao wakati wa mchakato wa uchaguzi huo.

Dorothy alisema kamati hiyo pia imemuomba Rais Samia Suluhu Hassan aingilie kati kuhakikisha hatua zilizobaki za uchaguzi huo zizingatie misingi ya haki kwa kufuata sheria na kanuni zinazoongoza uchaguzi.

Maeneo ambayo chama hicho kimemwomba Rais Samia aingilie kati ni kwenye uteuzi wa wagombea, upigaji kura, kuhesabu na wakati wa kutangaza matokeo.

"Kamati ya Uongozi Taifa ya ACT-Wazalendo imesikitishwa na mwenendo usioridhisha wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hasa kwenye uchukuaji na urejeshwaji fomu, ikiwamo baadhi ya wasimamizi kufunga ofisi, mfano Kondoa Vijijini, Newala, Tunduma na Ulyankulu. "Kukataa kupokea fomu za wagombea na kukataa maelekezo ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ya kuvipa vyama uhuru wa kuchagua ngazi ya chini ya kudhamini wagombea, mfano, kijiji cha Wari Ndoo, kata ya Machame Kaskazini, wilayani Hai, na maeneo mbalimbali ya jimbo la Ruangwa," alidai Dorothy.

Alisema kuwa pia kuna baadhi ya wagombea wao wanadai kupigiwa simu na watu wakiwatishia waliorejesha fomu wajitoe kuwa wagombea na kwamba jambo hilo limejitokeza kijiji cha Miuta, Tandahimba na mtaa wa Kanenwa, kata ya Kishiri, Nyamagana, mkoani Mwanza.

TANGAZO

KILIMANJARO
DRINKING WATER

A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company

Mshindi wa
**SUPERBRANDS AFRIKA MASHARIKI 2022-2024**








**Asanteni wateja wetu**
**Hii ni yetu sote**

kilimanjaro_drinking_water  kilimanjarodrinkingwater  kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422




Rais mstaafu Jakaya Kikwete (katikati) akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. bilioni moja kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, wakati wa hafla ya chakula cha jioni cha kuchangisha fedha za matibabu ya moyo kwa watoto wasio na uwezo wanaotibiwa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI). Hafla hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam. Pichani ni viongozi wengine wandamizi wa Benki ya NMB pamoja Naibu Spika wa Bunge, Mussa Hassan Zungu na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Suleiman Jaffo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Kikwete apongeza NMB kwa bil. 1/- za matibabu ya watoto JKCI

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete amekiri kuvutiwa na mchango mkubwa wa Benki ya NMB wa Sh. bilioni moja kati ya Sh. bilioni 2.71 zilizokusanywa wakati wa hafla ya kuchangisha fedha za matibabu ya watoto 1,500 wanaotibiwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Kikwete alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla hiyo iliyoandaliwa na JKCI kwa kushirikiana na Heart Team Africa Foundation (HTAF), lengo likiwa kukusanya fedha za matibabu ya watoto wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Kikwete alisema Sh. bilioni moja zilizotolewa na NMB, iliyotia saini makubaliano ya ushirikiano na JKCI ya kutoa kiasi hicho kwa miaka minne, kinakwenda kuongezea nguvu serikali inayopambania uamuzi wake wa kisera wa kuendelea kujenga uwezo wa ndani wa kutibu maradhi ya moyo.

"Gharama za kupeleka wagonjwa nje ni kubwa sana na huu ulikuwa ndio msukumo uliozaa uanzishwaji wa JKCI, leo taasisi imefikia hatua kubwa na bora katika matibabu ya moyo, ambayo serikali inagharamia asilimia 70 ya matibabu na familia kuachiwa asilimia 30 (sawa na Sh. milioni nne kwa mtoto), ambayo pia ni kubwa kwa walio wengi.

"Nimevutiwa na michango ya wadau wa afya, kipekee sana kwa mchango wa NMB. Pesa alizochangia dada'angu Ruth Zaipuna (Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB), ni nyingi mno, Sh. bilioni moja walizotoa zinakwenda kuokoa maisha ya takribani watoto 250 kati ya 1,500, wakiwamo 500 wanaohitaji operesheni ya haraka," alisema Kikwete.

Kikwete alipongeza serikali za awamu ya tano na sita kwa kuendelea kuwekeza katika shughuli za JKCI na kugharamia asilimia 70 za gharama za matibabu, ambapo taasisi imeendelea kuimarishwa kwa vifaa vya kisasa, huku akiwataka wadau zaidi kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali.

Akizungumza kabla ya kukabidhi hundi ya mfano yenye thamani ya Sh. bilioni moja, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Zaipuna, alimpongeza Rais mstaafu Kikwete kwa maono yake yaliyolenga kutatua changamoto za watanzania wanaosumbuliwa na magonjwa ya moyo na kuanzisha JKCI, ambayo sasa imekuwa tegemeo ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

"Benki ya NMB ipo hapa kuungana na wadau wetu katika maendeleo ya kijamii ili kuunganisha nguvu zitakazoleta nuru kwa watoto wetu, kwa kugusa mioyo yao na kuwatia matumaini kwa kuendelea kufanikisha upatikanaji huduma bora na nafuu za kitabibu, hasa kwa watoto wenye changamoto za moyo.

"Katika kuunga mkono jitihada hizi, hivi karibuni NMB tumetia saini makubaliano ya kuchangia Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne na leo tuko hapa kukabidhi hundi ya mfano yenye thamani hiyo, tukiamini kwamba mchango wetu utakuwa msaada mkubwa hasa kwa wazazi wanaoshindwa kumudu gharama za matibabu ya watoto wao.

"Licha ya mchango huu, NMB itashirikiana na JKCI, kuwezesha wataalamu wa taasisi hii kutoa elimu ili kuongeza ufahamu wa afya ya moyo kwa watanzania, pia tutawajibika kushiriki shughuli mbalimbali za upatikanaji fedha za matibabu ya watoto wenye magonjwa ya moyo JKCI," aliahidi Zaipuna.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge mbali na kumpongeza Rais mstaafu kwa maono yaliyozaa taasisi hiyo na uwekezaji mkubwa aliofanya wakati wa uongozi wake, alisifu mapinduzi makubwa ya kihuduma na kimfumo yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan anayeungwa mkono na wadau, ikiwamo NMB.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kuhakikisha 4R zake zinafanya kazi nzuri katika nyanja zote, lakini pongezi za kipekee ni kwako Rais mstaafu kwa kuwezesha wazo la kuwa na taasisi hii ambalo lilikuwapo tangu enzi za Rais wa Kwanza Julius Nyerere, lakini likakwama. Wewe ukaliibua na kulifanikisha.

"Ukajenga taasisi hii kwa msaada wa Serikali ya China, serikali yako ikitoa Sh. bilioni 11 na Serikali ya China ikitoa Yuan bilioni 18 na kufanikisha ujenzi wa JKCI ambayo imekuwa suluhu ya changamoto za moyo Afrika Mashariki, ambako tayari tumeshafanya zaidi ya operesheni 688,00 tangu mwaka 2015 ilipoanza," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya HTAF ambaye pia ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Mussa Zungu, alimshukuru Rais mstaafu Kikwete na kusema mchango wa kiongozi huyo wa zamani kwa sekta ya afya, hasa watoto wenye magonjwa ya moyo ni wa kipekee.

"Maono yako yameacha urithi wa kweli kupitia wazo lako la uanzishwaji JKCI, ambayo imekuwa kimbilio la wengi si tu hapa nchini, bali pia Afrika Mashariki na Kati. Hakika wewe ni mfano wa kiongozi anayejali afya za watu wake na kinachofanyika hapa ni mwendelezo utokanao na maono yako.

"Shukrani za dhati kwa Rais Samia katika kuboresha si tu miundombinu na vifaa tiba, bali pia kukubali kuchangia asilimia 70 ya gharama za matibabu ya watoto, ambao wanachangiwa katika hafla hii kupata asilimia 30 ya gharama hizo. Tunashukuru NMB kwa mchango wa Sh. bil. moja, lakini pia kwa washiriki na wachangiaji wote," alisema Zungu.

## Mbunge apata njia kuwasaidia vijana kuaga maisha magumu

**Na Frank Monyo**

MBUNGE wa Buchosa na mwandishi nguli wa vitabu, Eric Shigongo, amezindua kitabu cha 'Safari Yangu,' ambacho kinalenga kuwapa vijana matumaini na hamasa ya kujenga uchumi imara na kuendelea mbele licha ya changamoto za maisha.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho kilichoandikwa na Fatuma Maulid Juma, Shigongo alisema wakati umefika kwa vijana kubadilika kwa kuongeza maarifa ya kukabiliana na changamoto kwa kusoma vitabu ili viwasaidie.

Shigongo alisema mwandishi wa kitabu cha Safari Yangu alipitia shida na tabu nyingi katika maisha yake ambayo yamebeba ujumbe wenye lengo la kuwasaidia watanzania, hasa vijana wanaotafuta njia ya kutoka katika maisha magumu.

"Wakati mwingine Mwenyezi Mungu anatupitisha katika matatizo ili tuwe na moyo wa kuwasaidia wengine tukiwa tumefanikiwa, ninampongeza mwandishi wa kitabu cha Safari Yangu kwa kuonesha ujasiri kwa kuandika historia ya maisha yake ili wengine wajifunze kupitia yeye," alisema Shigongo.

Alisisitiza umuhimu wa watanzania kupendana na kusaidiana pamoja na kuoneshana fursa za maendeleo ili taifa lipige hatua na kufikia malengo husika.

Fatuma, mwandishi wa kitabu hicho, alisema amekiandika kwa ajili ya kutoa mchango kwa jamii, hasa kuwatia moyo wanaopitia katika matatizo.

Fatuma alisema kuwa katika maisha yake alipitia matatizo mengi, ikiwamo kushindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa ada ya shule.

"Sijawahi kukata tamaa, nilipambana na kupata matumaini ya kusonga mbele, leo hii mimi ni mtumishi wa Umoja wa Mataifa, ninaishi Marekani, kama ningekata tamaa nisingeweza kufika hapa nilipo," alisema.

Alieleza kuwa furaha yake ni kuona vijana wanaopitia changamoto mbalimbali za kimaisha wanafanikiwa na kurudi kuwainua wengine waweze kufikia malengo yao.

Alifafanua kuwa mapato ya mauzo ya kitabu cha Safari Yangu yatakwenda kuwasaidia watoto wenye uhitaji wanaoishi katika mazingira magumu katika taasisi ya RACAS Foundation.

Prof. Harun Nyagori anayefundisha katika vyuo vikuu mbalimbali vya tiba, aliwataka vijana kuwa wavumilivu wakati wanapitia changamoto mbalimbali katika maisha yao.

Prof. Nyagori alisema kwa Fatuma alipitia changamoo nyingi katika maisha yake, lakini hakukata tamaa, jambo ambalo lilimsaidia kufikia malengo na kupiga hatua kimaendeleo.

"Unapoanguka unapaswa kuinuka na kusonga mbele, taasisi na jamii kwa ujumla tuwe na utamaduni wa kuendelea kushirikiana kuwasaidia watu wenye uhitaji kwa kuwashika mkono," alisema Prof. Nyagori.

TANGAZO

# TAARIFA KWA UMMA

TANGAZO HILI LIMEIDHINISHWA NA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA)

## PROGRAMU YA HATIFUNGANI YA MUDA WA KATI YA BENKI YA AZANIA PLC: TOLEO LA KWANZA - BONDI YANGU

AZANIA BANK
*Benki Inayozidi Matarajio*

Benki ya Azania inatoa taarifa kwa umma kwamba Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa Programu ya Miaka Mitano ya Hatifungani yenye jumla ya Shilingi 100,000,000,000 (Shilingi za Kitanzania (Tsh) Billioni Mia Moja). Hali kadhalika, CMSA imeidhinisha Toleo la kwanza la Programu ya Hatifungani (Bondi Yangu), lenye jumla ya Tsh Bilioni 30 (ikiwa na uwezo wa kuchukua ziada ya Tsh Bilioni 15), itakayowezesha kupata fedha za kutekeleza miradi yenye malengo ya kimkakati kwenye sekta za uchumi zenye tija.

**Taarifa ya Hatifungani Toleo la Kwanza – Bondi Yangu**

| Mtoaji: | Azania Bank Plc |
|---|---|
| Jumla ya Kiasi: | TSH 100,000,000,000 (Shillingi za Kitanzania Bilioni Mia Moja) |
| Kiasi cha Toleo ya Kwanza | TSH 30,000,000,000 (Kiasi kitakachozidi kitachukuliwa hadi Tsh 15,000,000,000) |
| Riba iliyopangwa (Kuponi): | 12.5% kwa mwaka itakayolipwa mara nne kwa mwaka |
| Kiwango cha chini: | TSH 500,000 (Shillingi za Kitanzania Laki Tano) |
| Tarehe ya Toleo: | 16 Desemba 2024 |
| Tarehe ya Kuiva kwa Hatifungani: | 16 Desemba 2028 |
| Tarehe za Malipo ya Riba: | 16 Machi, 16 Juni, 16 Septemba, 16 Desemba |
| Riba ya Hatifungani: | Asilimia 12.5 kwa mwaka. Riba isiyobadilika itakayolipwa mara nne kwa mwaka |
| Muda wa Hatifungani: | Miaka 4 |
| Kodi: | Hatifungani haina kodi ya zuio |
| Kuorodheshwa DSE: | Hatifungani itaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |

Uwekezaji unafanyika kwa kujaza Fomu ya Maombi inayopatikana kwenye matawi ya Benki ya Azania; kwa mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam waliopewa leseni na Mamlaka ya Masoko na Dhamana (CMSA); au kwenye tovuti ya Azania **www.azaniabank.co.tz**

**Maombi yatakamilishwa kwa kufanya malipo katika akaunti za benki ya Azania zilizoainishwa hapo chini:**

1. Akaunti ya Kulipia

| | |
|---|---|
| Azania Bondi Yangu Collection Account | 033000001881 |

| S/n | Tukio | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. | Tarehe ya kuidhinishwa kwa hatifungani na CMSA | Alhamisi, 26 Sep 2024 |
| 2. | Tangazo la hatifungani kwa Umma | Jumatatu, 04 Nov 2024 |
| 3. | Kuanza kupokea maombi ya ununuzi wa hatifungani | Jumatatu, 04 Nov 2024 |
| 4. | Mwisho wa kupokea maombi ya ununuzi hatifungani | Ijumaa, 06 Des 2024 |
| 5. | Mgao kwa wawekezaji | Alhamisi, 12 Des 2024 |
| 6. | Kutangaza matokeo ya mauzo ya hatifungani | Ijumaa, 13 Des 2024 |
| 7. | Tarehe ya toleo | Jumatatu, 16 Des 2024 |
| 8. | Kuwasilishwa kwa rejista CSDR | Jumanne, 17 Des 2024 |
| 9. | Kuingiza CDS kwenye mfumo wa DSE | Jumanne, 17 Des 2024 |
| 10. | Kuorodheshwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) | Jumatano, 15 Jan 2025 |
| 11. | Mwisho wa Hatifungani | Jumatatu, 16 Des 2028 |

Wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenye leseni kutoka Mamlaka ya Masoko, Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

**Imetolewa Na:**
Mkurugenzi Mkuu,
Azania Bank Plc,
Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
P.O BOX 32089
Dar es Salaam, Tanzania.

Connecting all your banking needs.

*customercare@azaniabank.co.tz | 0800 110 210*

www.azaniabank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bodi ya Ligi inalea timu kutumia milango isiyo rasmi viwanjani

**KWA** mara nyingine tena Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, imezitoza faini timu ambazo zimekuwa na tabia ya kupitia milango isiyo rasmi wakati wa kuingia uwanjani kwenye michezo yao.

Mwishoni mwa juma, Yanga ambayo kwa misimu kadhaa imekuwa ikifanya kosa hilo, ilipigwa faini ya Sh. milioni 13, ambapo pamoja na makosa mengi, lakini lipo lile la kutumia mlango usio rasmi kuingilia uwanjani siku ya mchezo, kinyume cha kanuni ya 17:62 ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za mchezo, ambapo kosa hilo faini yake ni Sh. milioni kumi.

Pili imetozwa faini ya Sh. milioni moja nyingine kwa kosa la kukataa kutumia chumba maalumu cha kubadilishia nguo kinyume cha kanuni ya 17:62, na kosa la tatu imetozwa pia Sh. milioni moja kutokana na kuwakilishwa na kocha mkuu pekee kwenye mkutano na wanahabari kinyume cha matakwa ya kanuni ya 17:58 ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za mchezo, inayotaka aambatane na nahodha ama mchezaji mwenye ushawishi kikosini.

Hatutaki kwenda kwenye kosa la nne ambalo limefanywa na meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, katika mchezo wao dhidi ya Coastal Union na kisha kutozwa faini ya Sh. milioni moja na kumfungia michezo mitatu, badala yake tunataka kwenda kwenye kosa sugu la kutotumia mlango rasmi.

Labda tuseme Bodi ya Ligi imeruhusu mwanya huo makusudi ili kuingiza fedha zinazopatikana kwa faini, lakini kama lengo ni kukomesha inaweza kabisa.

Je, inawezekana? Ndiyo kwa sababu Bodi ya Ligi ilitupilia mbali maoni ya baadhi ya wadau wa soka wakati wa kutuma mapendekezo ya mabadiliko ya kanuni za Ligi Kuu kabla ya msimu kuanza, ambayo yalipendekeza timu zinazoendeleza tabia hiyo kukatwa pointi pamoja na faini.

Adhabu inapotolewa kwa mwenye kosa na kisha akarudia kutenda kosa lile lile kila mara, basi ujue haimgusi wala kumuumiza, badala yake inatakiwa ibadilishwe.

Timu zenye tabia hii zingekatwa angalau pointi moja tu, zisingerudia kosa hilo. Lakini pia Bodi ya Ligi inaonekana kulea jambo hili kwa kuwa hata kama si kukatwa pointi inaweza kabisa kuweka ulinzi wa kutosha wakati timu zinaingia uwanjani ili kuhakikisha zinatumia mlango rasmi.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba inafahamu kabisa muda ambao wachezaji wanatakiwa kuwasili, hivyo ingeweza kuweka walinzi wa kulinda milango yote, na mingine kuifunga kabisa, hilo lisingeweza kutokea.

Milango yote ikifungwa kwa muda ule tu ambao timu zinatakiwa kuwa zimefika, halafu baada ya hapo ikafunguliwa, hakuna timu ambayo ingeweza kufanya hivyo, vinginevyo labda kama inaachia kwa makusudi ili kuingiza fedha kwa njia ya kutoza faini.

Ifike wakati Bodi ya Ligi ilisaidia Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kuilinda ligi hii kuwa na sifa zinazoendana na nafasi yake ya kuwa namba sita kwa ubora Afrika.


Haiwezekani ligi bora kama hii bado kuwe na timu, tena kubwa, zinapitia mlango usio rasmi na sababu kubwa hapa utagundua ni kile ambacho yenyewe Bodi ya Ligi imekuwa ikibainisha kuwa ni viashiria vya imani zinazodaiwa kuwa za kishirikina.

Tunataka kuona sasa Bodi ya Ligi ikidhibiti mambo haya ili kuiheshimisha ligi yetu, na msimu huu pia ukiwa wa mwisho, badala yake kuwekwe kanuni za kukata pointi hata moja tu sambamba na faini inazozitaka ili kukomesha vitendo hivyo.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Silaha ya mwamuzi uwanjani ni kadi si ukali, mikono, maneno

**LILIKUWA** ni jambo la kushangaza, kuhuzunisha na kuchekesha kwa wakati mmoja pale mwamuzi Omri Mdoe alipoonekana kumsukuma mchezaji Yusuph Dunia katika mchezo wa Ligi Kuu kati ya Mashujaa na Simba, uliochezwa Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma.

Mdoe alionekana kufanya tukio hilo akiwa katika harakati za kumtuliza Dunia aliyeonekana kulalamika kwa kutokubaliana naye, alipoamuru faulo ilekezwe kwao baada ya Joshua Mutale kufanyiwa madhambi.

Mdoe alifanya hivyo mara mbili na baadaye wachezaji wa Mashujaa wakaja kumuondoa mwenzao.

Mmoja wa watu walio kwenye Kamati ya Waamuzi ambaye hakutaka jina lake litajwe kwa sababu haruhusiwi kuliongelea suala hilo kimaadili, amesema kamati hiyo inaweza kufanya kazi ya kupitia tukio hilo na kuona kama alifanya sahihi au la.

Ni tukio ambalo limezua gumzo kubwa sana kwa mashabiki na hasa kwenye mitandao ya kijamii, huku wengine wakitengeneza vibonzo.

Ukiangalia kwenye mchezo huo utagundua mwamuzi huyo aliogopa kutoa kadi si kwenye tukio hilo tu bali kwenye mchezo mzima ambao ulitawaliwa na matumizi ya nguvu wakati mwingine kupita kiasi.

Cha ajabu ni kwamba kulikuwa na kadi moja tu ya njano kwenye mchezo huo licha ya kwamba takwimu zilionesha idadi kubwa ya madhambi.

Hata Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alilalamika juu ya wachezaji wake kuchezewa vibaya, lakini mwamuzi hakuchukua hatua stahiki.

Ndiyo maana haikushangaza kuona alishindwa kumuonesha mchezaji kadi badala yake akaamua kumsukuma naye. Ina maana Mdoe hajui kuwa kadi ndiyo silaha yake uwanjani na si mdomo, mikono au ukali? Hapa inashangaza kweli.

> **Ndiyo maana haikushangaza kuona alishindwa kumuonesha mchezaji kadi badala yake akaamua kumsukuma naye. Ina maana Mdoe hajui kuwa kadi ndiyo silaha yake uwanjani na si mdomo, mikono au ukali? Hapa inashangaza kweli.**

Hii inaonyesha kuwa ni mmoja wa waamuzi ambao hawajiamini, au aliamua tu kuwa mechi hiyo asioneshe kadi nyingi za njano kwa sababu anazozijua yeye.

Kwa waamuzi wanaojua kazi zao na wanaojiamini, wakati mchezaji anakuja angepeleka tu mkono kwenye mfuko wa chini kuonesha kama anatoa kadi nyekundu, sidhani mchezaji yule angefika hadi pale alipo.

Nitoe pongezi kwa mwamuzi Ahmed Arajiga na wasaidizi wake waliochezesha mchezo kati ya Yanga na Azam FC, na waliochezesha mchezo kati ya Singida Black Stars na Yanga pale Uwanja wa New Amaan Complex visiwani Zanzibar, kwani walionekana kuchezesha kwa mamlaka, huku wakiwadhibu kwa kadi kila kosa lililoonekana linastahili kufanya hivyo.

Wakakati mwingine wachezaji ni kama wanafunzi tu au watoto, hufanya jinsi ambavyo anayewaogoza alivyo.

Kama ni dhaifu basi wanaweza kumpelekesha, lakini akiwa mkali wanatii shuruti, na ndiyo ilivyokuwa.

Na mara nyingi mwamuzi anayeamua tukio kwa usahihi huwa hana kazi kubwa ya 'kubalansi' mchezo kwani huacha mchezo ujiendeshe wenyewe, anachofanya yeye ni kuamua matukio kwa jinsi yanavyojitokeza tu.

Wale wa 'kubalansi' inafika wakati mechi inawashinda kwa sababu mwanzo aliacha huku, linatokea jambo lingine kubwa upande mwingine anashindwa kufanya maamuzi kwa sababu awali aliacha upande mwingine.

Kamati ya Waamuzi, Chama cha Waamuzi nchini, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), na Bodi ya Ligi (TPLB), inadibi kufanya uchunguzi kama baadhi ya waamuzi wanafanya hivi kwa shinikizo kutoka mahali fulani, uwezo mdogo, presha ya mchezo, malipo madogo, wanacheleweshewa posho zao au kuna nini?

# Kiboko auawa, wananchi wagawiwa nyama

**Na Mwandishi Wetu,** MAGU

KIBOKO aliyehatarisha maisha ya watu katika kijiji cha Ilungu, kata ya Nyigogo, wilayani Magu, ameuawa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) baada ya kuvamia mashamba ya wakulima wanaofanya shughuli za kilimo cha mpunga na mahindi katika kitongoji cha Moa, wilayani humo.

Tukio hilo lilitokea jana baada ya wananchi hao wanaolima kando ya Ziwa Victoria kushindwa kumdhibiti kiboko huyo na hivyo kuomba msaada TAWA ambao walifanikiwa kumuua kwa kumpiga risasi.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya Ofisa Mifugo wa Kata ya Nyigogo, Hamis Gido kudhibitisha kuwa nyama hiyo ni salama kwa matumizi ya binadamu, baadhi ya wananchi walishukuru serikali kwa kuwatatulia changamoto hiyo.

Walisema eneo hilo pamekuwapo na usumbufu wa kiboko mara kwa mara lakini sasa kutokana na kiboko huyo mmoja kuuawa wanaamini hata wengine waliokuwa karibu watakimbia.

Mmoja wa wananchi hao, Pungwe Wilson ambaye pia ni mkulima, alisema kuwa kwa muda mrefu pamekuwa na kilio cha wananchi kuhusu wanyama waharibifu wanaotokea ziwani.

"Lakini sasa tunashukuru serikali kwa kumuua mnyama huyu ambaye pia amekuwa hatari hata kwa maisha yetu sisi wakulima," alisema Wilson na kuungwa mkono na wananchi wengine, wakiwamo Magina Mbute na Ngubi Mega.

Awali Askari wa Uhifadhi Mwandamizi kutoka TAWA, Loiruck Moses alisema wamefanikiwa kukabiliana na mnyama huyo ikiwa ni zoezi endelevu la kuwadhibiti wanyama waharibifu.

Alitoa wito kwa wananchi pindi wanapokabiliana na wanyamapori wanapoonekana mahali popote, watoe taarifa ili askari wafike kukabiliana na wanyama hao.

Ofisa Mifugo wa Kata ya Nyigogo, Hamisa Gido alisema ni suala lililozoeleka katika maeneo mengi pindi mnyama kiboko anapouawa na nyama yake kupimwa na kuonekana haina dosari yoyote, hugawiwa kwa wananchi ili wapate kitoweo.

Mhifadhi Wanyamapori Wilaya ya Magu, Christopher Christian alisema wanyamapori hao wamekuwa wasumbufu kwa wananchi wa kijiji hiyo lakini wanashukuru TAWA kwa kushirikiana pamoja kudhibiti mnyama huyo.

# Utafiti wabaini tatizo la akili kwa watu wanaoishi na VVU

**Na Christina Mwakangale**

UTAFITI umebaini Watu Wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi na Ukimwi (PLWHA) ni miongoni mwa makundi yanayokumbwa zaidi na magonjwa ya akili, ukiwamo wasiwasi kulinganishwa na makundi mengine.

Utafiti uliofanywa na Hospitali ya Rufani ya Kanda - Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC) kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na kuhusisha watu 593 (wanaume 164), umebaini kuna tatizo hilo.

Bingwa wa Magonjwa na Afya ya Akili KCMC, Dk. Frank Kiwango, akizungumza na Nipashe jana mara baada ya kuwasilisha andiko la utafiti kupitia Jumuiya ya Wadau wa Afya ya Akili Tanzania (TMH-CoP) ECHO, wasilisho likiandaliwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) mwishoni mwa wiki iliyopita.

"Kuna athari kwa wanaougua ugonjwa huo kwa sababu wanaweza kukata tamaa na kushindwa kutumia dawa zao za ARV, mtu akawa na wasiwasi zaidi na kitaalamu ataendelea vibaya. Kwa ujumla, maisha yatakuwa changamoto, hasa kwenye kuishi," alisema.

Dk. Kiwango alisema walifanyiwa utafiti Septemba hadi Oktoba mwaka jana na matokeo kutolewa hivi karibuni katika kundi la PLWHA 593, watu 74 (asilimia 12) wana dalili ya ugonjwa wa wasiwasi, akisema ni idadi kubwa ambayo inahitaji kufikiwa kwa elimu.

"Ni kwa sababu watu wenye VVU wako hatarini kupata magonjwa hayo kama wasiwasi, sonona kwa hiyo tukaona kwa kuwa wamo hatarini na utafiti kadhaa wa nje umeonesha kwamba wako hatarini kuliko ambao hawana magonjwa sugu.

"Tukaona tufanye utafiti kwenye eneo hilo. Tumefanya utafiti mjini Moshi, mkoa wa Kilimanjaro katika vituo vya CTC vinne, ambavyo vinatoa huduma za VVU. KCMC; Hospitali ya Mkoa Mawenzi na vituo vya afya," alisema.

Bingwa huyo ambaye ndiye mtafiti mkuu kwenye utafiti huo, alisema baada ya kupata matokeo hayo, tayari mchakato wa kutoa elimu kupitia programu za afya elimishi umeanza, kama vile katika vyombo vya habari na makongamano.

"Wito kwa jamii ili kundi hili lisiingie katika tatizo, liweze kuangaliwa kwa jicho la ziada na kuwapo kuchunguza magonjwa ya akili, ili kuwahi kupata huduma stahiki mapema," alishauri.

Alirejea ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2021 inayoonesha kuwa takribani watu wazima milioni 36 wanaishi na VVU/UKIMWI kwa mwaka huo. Kati yao, theluthi mbili wako barani Afrika. Pia PLWHA wapatao milioni 1.6 wanatoka Tanzania (WHO 2022).

Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Nuruel Kitomary, alisema kuwa na ugonjwa huo kunaweza kusababisha mtikisiko wa hisia, jambo linaloweza kuwasababishia watu wa kundi hilo kuathiri mtiririko wa matibabu.

"Wasiwasi unaweza kushusha kinga ya amwili, tukumbuke pia wasiwasi kila binadamu anao ila ukizidi inapaswa kuingia katika matibabu.

Kukaa kimya katika hili na ukosefu wa elimu kuna athari," bingwa huyo alihadharisha.


CBT
Bank

**Uteuzi wa Bw. Godfrey Ng'urah kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Ushirika ya Tanzania (CBT)**



Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Benki ya Ushirika ya Tanzania (CBT) ina furaha kutangaza uteuzi wa Bw. Godfrey Joel Ng'urah kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Ushirika ya Tanzania, kuanzia Oktoba 2024. Bw. Ng'urah ni mtaalamu aliyebobea katika sekta ya benki, akiwa na zaidi ya miaka 18 ya uzoefu wa mafanikio katika sekta ya benki na ushirika. Ni mbobezi wa masuala ya mageuzi ya biashara, mabadiliko ya kidijitali, usimamizi wa mikopo, na usimamizi wa miradi ya kimkakati. Kwa miaka yote aliyohudumu katika sekta ya benki na ushirika, ameonesha umahiri mkubwa katika kuleta matokeo chanya katika kufanikisha malengo ya taasisi na ya kisekta.

Kabla ya uteuzi huu, Bw. Ng'urah alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL), ambapo aliiongoza mageuzi ya kuifanya kuwa benki kamili ya kibiashara inayojulikana sasa kama Benki ya Ushirika ya Tanzania (CBT). Juhudi zake KCBL ziliimarishwa zaidi kupitia muungano wa mafanikio na Benki ya Wananchi ya Tandahimba (TACOBA), uliopanua wigo wa soko na kuboresha ufanisi wa kiutendaji. Maono ya kimkakati ya Bw. Ng'urah na uongozi wake sio tu umeimarisha muundo wa mtaji wa CBT, bali pia umeiweka kwenye njia sahihi ya ukuaji endelevu na ushindani katika soko la benki.

Kabla ya kujiunga na KCBL, Bw. Ng'urah alifanya kazi kwa mafanikio makubwa ndani ya Benki ya CRDB, ambako alihudumu kama Meneja wa Mabadiliko ya Biashara, akiongoza miradi ya mageuzi iliyosaidia kuimarisha muundo wa idara ya wateja wadogo na wa kati, kuboresha michakato, na kuimarisha njia za utoaji huduma katika mtandao wa matawi ya Benki ya CRDB. Hapo awali, alihudumu kama Meneja Mwandamizi wa Mahusiano kwa Wajasiriamali Wadogo na Kati, ambapo alichangia katika kuendeleza na kutekeleza mkakati wa biashara, kukuza ukuaji wa mikopo, na kuhakikisha ubora wa mikopo.

Bw. Ng'urah ana shahada ya Uzamili ya Biashara katika Usimamizi wa Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, ni Mtaalamu wa Benki aliyethibitishwa (CPB), na Mkurugenzi aliyethibitishwa, baada ya kukamilisha Programu ya Uongozi wa Juu katika Shule ya Biashara ya Strathmore (SBS). Uzoefu wake mkubwa na uwezo wa kipekee wa uongozi, unamfanya kuwa mtu sahihi katika kuiongoza CBT katika hatua yake inayofuata ya ukuaji na mafanikio.

Bodi ya Wakurugenzi ina imani kuwa chini ya uongozi wake, Benki ya Ushirika ya Tanzania itaendelea kustawi na kuongeza mchango wake katika sekta ya benki nchini.

Tunawakaribisha kuungana nasi kumpongeza Bw. Ng'urah kwa uteuzi wake na kumtakia kila la heri katika nafasi yake mpya.

Prof. Gervas Mathias Machimu
**Mwenyekiti wa Bodi**
**Benki ya Ushirika ya Tanzania (CBT)**

# Maelfu wanufaika na semina za ujasiriamali Programu ya Imbeju

**Na Mwandishi Wetu**

NIMEFURAHI kufika Katavi. Hii ni mara yangu ya kwanza kufika huku. Nimependa ubora wa barabara. Ukiangalia barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mpanda, utaiona dhamira ya dhati ya serikali kuboresha maisha ya Watanzania. Sisi Taasisi ya CRDB Bank Foundation tumekuja huku kuwaletea wananchi wenzetu fursa za kukuza kipato chao binafsi," anasema Ibrahim Isack, Ofisa Imbeju aliyeshiriki awamu ya kwanza ya ziara ya uelimishaji chini ya Programu ya Imbeju.

Isack ni miongoni mwa Watanzania wachache waliopata bahati kuzunguka mikoa kadhaa ya nchi na kuona juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau kusogeza maendeleo kwa wananchi katika nyanja tofauti na kwa uzoefu aliopata katika ziara hii, anasema jamii inahitaji elimu ya ujasiriamali kujikomboa kiuchumi.

"Nimezunguka kuanzia Katavi, Rukwa halafu Songwe mpaka Mbeya. Kote kuna ardhi inayokubali kilimo na misitu mingi rafiki kwa ufugaji, ukiwamo wa nyuki. Watu wanajituma kwa kuzichangamkia fursa zinazowazunguka ingawa ni kwa kiasi kidogo. Wanahitaji uwezeshaji ili kunyanyuka zaidi," anasema Isack.

Katika ziara hiyo ya uelimishaji, Isack pamoja na maofisa wenzake kutoka makao makuu ya CRDB Bank Foundation inayotekeleza Programu ya Imbeju, wamezunguka katika kata na wilaya nyingi za mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kutoa mafunzo ya ujasiriamali, elimu ya fedha pamoja na kuwafungulia washiriki akaunti ya Imbeju.

Katika vijiji, kata na wilaya ambako Isack na wenzake walipiga kambi kwa siku 35 za kuzunguka, anasema walitoa elimu iliyokusudiwa huku wakishirikiana na kila mdau muhimu ili kuwafikia watu wengi zaidi.

"Wananchi wameamka. Kwenye kila halmashauri utakayokwenda nchini, kuna vikundi vingi vya wajasiriamali. Juhudi za kuanzisha vikundi hivi zinatokana na wananchi kutambua kwamba nguvu zao zipo kwenye umoja wao ambao unatambuliwa na serikali, sekta binafsi hata taasisi za dini zenye programu za kuwawezesha wananchi," anasema Isack.



Ofisa Imbeju, Ibrahim Isack akitoa elimu kwa wanawake wajasiriamali waliomletea nyaraka za kikundi chao walipohudhuria semina ya Imbeju wilayani Tanganyika, mkoani Katavi hivi karibuni.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### PROGRAMU YA IMBEJU

Imbeju, neno la kibantu linalomaanisha mbegu, ni programu inayotekelezwa na Taasisi ya CRDB Bank Foundation ili kuwainua wajasiriamali wadogo nchini kwa kukuza biashara zao kupitia huduma za benki.

Programu hiyo iliyozinduliwa mwaka jana, tayari imewafikia maelfu ya wananchi kupitia semina zake na kuwanufaisha baadhi ya washiriki kwa kuwajumuisha kwenye huduma za benki tayari kuanza safari ya kujenga uchumi wa kudumu utakaokuwa endelevu kutoa kwao na vizazi vijavyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa anasema wajasiriamali wengi wadogo kuanzia wakulima, wachimbaji madini, mama lishe, mafundi washona nguo na wengine wa aina hiyo hawatumii huduma za benki, hivyo kukosa nyenzo muhimu za kukuza biashara zao pindi zinapohitaji mtaji wa ziada.

Kwa kulitambua hilo, Tully anasema Taasisi ya CRDB Bank Foundation ilikuja na Programu ya Imbeju ili kutatua changamoto zilizopo, hivyo kutoa nafasi kwa Watanzania wenye kipato kidogo nao kunufaika na uwezeshaji unaotolewa na benki katika kukuza biashara.

"Kwenye Programu ya Imbeju tunafanya vitu vinne. Kwanza tunawafundisha wananchi kuhusu ujasiriamali halafu tunawapa elimu ya fedha. Wakishaelewa sasa tunawafungulia akaunti ya Imbeju ndipo wanakidhi kupata mtaji wezeshi. Mtaji wezeshi huu unaanzia Sh. 200,000 mpaka Sh. milioni 10 ingawa kuna uwezekano wa kuongezeka kulingana na uhitaji," anasema Tully.

Katika ujasiriamali, Tully anasema msisitizo unaotolewa kwa washiriki ni kuongeza vyanzo vya mpato kutoka na shughuli wanazozifanya. Katika kila eneo, anasema wananchi wanatakiwa kuangalia fursa zilizopo na kuzichangamkia ili kuimarisha kipato binafsi.

Kwenye kila biashara, anasema mjasiriamali anatakiwa kuangalia namna anavyoweza kuongeza thamani itakayompa kipato cha ziada. Fundi cherehani kwa mfano, anaweza kuongeza vitambaa na vifaa vya kushonea kwenye eneo lake na kwa kufanya hivyo, atakuwa ameongeza vyanzo vya mapato. Mteja akija atamlipa fedha ya ufundi, ununuzi wa kitambaa pamoja na vifaa vya ushonaji tofauti akiwa anashona tu.

Baada ya kuimarisha vyanzo hizi vya mapato, ni muhimu kujua matumizi sahihi. Tully anasema wahudhuriaji semina ya Imbeju wanaelezwa umuhimu wa kulinda na kuendeleza mtaji na kujiwekea akiba itakayosaidia kukuza au kuanzisha biashara nyingine ili kuimarisha kipato cha mhusika.

Kwa mjasiriamali mwenye nidhamu katika matumizi ya fedha ambaye atajenga utaratibu wa kujiwekea akiba, atahitaji kuwa na akaunti ya Imbeju ambayo haina makato ya kila mwezi wala gharama za uendeshaji.

"Mjasiriamali aliyehudhuria semina zetu au aliyeelimishwa na mwanakikundi mwenzake aliyehudhuria, akiwa na akaunti ya Imbeju anakidhi sifa za kupata mtaji wezeshi. Watu wengi wanachangamkia fursa ndio maana tuliona kuna haja ya kwenda katika mikoa yote nchini kufikisha elimu hii na kuwawezesha wajasiriamali," anasisitiza Tully.

Kuhusu ziara ya maofisa Imbeju wanaozunguka mikoani kutoa elimu, mkurugenzi huyo anasema ni mkakati wa kuhakikisha kila anayestahili kunufaika na Programu ya Imbeju nchini anafikiwa na kuwezeshwa.

Tully anasema "Agosti 31 tulizindua Imbeju roadshow tukianzia mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Malengo yetu ni kuzunguka nchi nzima. Tumekamilisha awamu hiyo ya kwanza na sasa tunajiandaa kwenda awamu ya pili katika mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya Magharibi."

Tangu kuzinduliwa kwa Programu ya Imbeju, Tully anasema zaidi ya wanachi 600,000 wamepata mafunzo yanayotolewa na maelfu kati yao kunufaika na mitaji wezeshi ya kukuza biashara zao.

### WASEMAVYO WANANCHI

Siyo mafunzo ya ujasiriamali au elimu ya fedha pekee ambayo washiriki wa semina za Imbeju wanafurahia, bali pia akaunti ya Imbeju inayowapa uhakika wa kutunza fedha zao.

Mratibu wa Vicoba Wilaya ya Songwe, mkoani Songwe, Aziz Kigaza anasema kwa mtindo waliokuwa nao kwenye Vicoba wa kugawana fedha mkononi, ulikuwa hatari kwao lakini kwa utaratibu wa kuwa na akaunti benki utawasaidia wengi kuepuka uhalifu wanaoweza kufanyiwa.

"Tulikuwa na utaratibu wa kupeana fedha mkononi. Yupo mwanachama mmoja ambaye alichukua mkopo wa Sh. milioni nne. Usiku wa siku hiyo alivamiwa na watu waliomkata mkono na kuondoka na fedha alizokuwa nazo. Ni jambo la kusikitisha sana. Kuna watu wenye tamaa wanaoweza kufanya chochote wakiona fedha," anasema Kigaza.

Fatuma Rajabu, mkazi wa mjini Chunya, anasema ni furaha kwake kumiliki akaunti ya benki baada ya kuhudhuria semina ya Imbeju.

"Sikuwahi kuwa na akaunti ya benki. Sasa hivi ninajiona nami ni sehemu ya watu wanaofanya mambo yao kwa umakini. Nitakuwa ninaweka akiba yangu sehemu salama kuanzia sasa," anasema Fatuma ambaye ni mama lishe.

### SERA ZA SERIKALI

Katika mikakati ya kuwawezesha wananchi kukabiliana na changamoto za kiuchumi wanazokutana nazo kila siku, mwaka 2004 serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi pamoja na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji. Haya yalifanyika kwa lengo la kuhakikisha watanzania wanamiliki uchumi wao.

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi inayotekelezwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (NEEC) kwa kushirikiana na wadau wengine, inatoa mwongozo wa uwezeshaji kulingana na mazingira ya sekta husika. Kila mwaka, serikali huratibu na kufuatilia utekelezaji shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Baraza linatekeleza jukumu hilo kwa kukuza na kusaidia shughuli za kiuchumi zinazoanzishwa na kuendeshwa na watanzania, kuwapa watanzania fursa ya kushiriki shughuli za kiuchumi na kuwahimiza watanzania kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi.

Tathmini ya utekelezaji sera hii kwa mwaka 2021/22 inaonesha Tanzania ina taasisi za fedha 44,441, zikiwamo 166 zilizosajiliwa mwaka 2022/23. Taasisi hizi ziliwakopesha jumla ya wateja 5,035,031.

Haya yote yanafanywa kwa lengo la kupunguza umasikini katika jamii na kujenga taifa lenye uchumi endelevu. Wanufaika wakuu wa huduma za uwezeshaji wananchi ni wakulima, wavuvi, wafugaji, wenye viwanda, wafanyabiashara, wanamichezo, wasanii, wabunifu, machinga na watumishi katika sekta ya umma na sekta binafsi.



Baadhi ya wachimbaji wadogo katika Mgodi wa Mwime wakiwa wameketi juu ya mifuko yenye mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu wakitafakari juu ya kufungwa mgodi huo kutokana kushidwa kuelewa mipaka ya bomba la mafuta linalopita katika mgodi huu likitokea Uganda hadi Tanzania. **PICHA: MOHABU DOMINICK.**

# Wanawake vinara waibua kero vijijini

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WANAWAKE vinara wa mabadiliko ya maendeleo, kiuchumi na kifkra, wakazi wa vijiji vya Naibili na Majengo, kata ya Biriri, wilaya ya Siha, wameibua mambo manne ambayo ni kero kwa wanajamii, wakiwamo wakaguzi wa umeme wa majumbani wa Shirika la Umeme (TANESCO) kuwatoza Sh. 30,000 ili kupata huduma hiyo.

Suala linalowahusu wakaguzi hao (surveyor), ni miongoni mwa kero zilizojibiwa na kurejeshea tabasamu kwa wanawake hao baada ya kupatiwa ufumbuzi na serikali.

Akiwasilisha ajenda za wanawake hao juzi katika mkutano maalumu wa utatuzi wa kero uliofanyika Kijiji cha Naibili, ukiwahusisha viongozi wa sekta mbalimbali serikalini, kiongozi wa jopo la wana vikundi vya wanawake, Mary Manjano, alisema lengo la kuita mkutano huo ni kupata majibu ya kina ya kero za maji, nishati, afya, barabara na elimu.

"Tumeandaa hoja zetu na kuita viongozi kutoka serikalini kupata mwafaka na vitu gani vifanyike ili jamii katika vijiji hivi ipige hatua zaidi kimaendeleo na hasa kiuchumi. "Tunashukuru tumepata ufumbuzi, kwa sababu tumekuwa na changamoto kubwa kwenye kuunganisha umeme majumbani na ule wa biashara. Tumekuwa tukitozwa na wakaguzi/wakadiriaji wa TANESCO Sh. 30,000 za 'surveyor' ili kupata huduma hiyo."


Kuhusu gharama kubwa za matumizi ya umeme wa luku, Ruwaichi Shirima, alisema: "Tumepata majibu ya kuturidhisha kwamba wale wanajamii wanaotumia chini ya uniti 75, tutarekebishiwa uniti kwenye mita zetu; kwa hiyo tutakuwa tunanunua uniti moja kwa Sh. 100, jambo ambalo limetupa faraja kubwa."

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Siha, Ismail Sallu, akijibu hoja za wananchi hao, aliwataka wote wanaoona matumizi yao ya umeme yanashida kwenye viwango vya tariff, wajiorodheshe kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji husika na majina yao yapelekwe kwake kupatiwa ufumbuzi.

Kuhusu wanaopita mitaani na kutoza wananchi Sh. 30,000 ili kuwasaidia kuunganishiwa umeme, Sallu, amewashauri kuwaripoti TANESCO mara moja ili hatua za kuwabaini zichukuliwe.

Katika mkutano huo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Naibili (VEO), Melchiory Moiti, alilishukuru Shirika la kiraia la TUSONGE CDO, kwa kuwa mkono wa pili wa serikali, likitoa elimu kwa wanawake, hasa uwekezaji katika vikundi vya kiuchumi kama vikoba, utunzaji wa fedha na uanzishwaji wa miradi ya kiuchumi.

"Kupitia TUSONGE CDO, jamii yetu imepona kutokana na kupata elimu ya uhifadhi wa mazingira, suala la ukatili, hususani mimba za utotoni, vipigo na ukatili wa kingono. Changamoto hizo sasa zimekuwa zikitatuliwa kirahisi kuliko ambavyo sisi tungetatua wenyewe." Tunamshukuru Mungu kwa Shirika la Tusonge kutupa mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali, kilimo na elimu ya kujitambua, ambayo imetufanya sisi kama wanawake kutambua haki zetu kimsingi, lakini na kuzichakata na kuona ni wapi tuwasilishe hoja zetu. Gilbert Owen ambaye ni Ofisa Ufuatiliaji na Tathimini wa Tusonge CDO, akizungumza katika mkutano huo, aliipongeza serikali akisema imekuwa ikifanya vizuri kuchukua hatua katika kila jambo linaloibuliwa na wananchi wa Kata hiyo.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA
*(AT ARUSHA)*

CRIMINAL CASE NO. 25584 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

AFROIL INVESTMENT LIMITED................................ACCUSED PERSON

To:
Managing Director
Afroil Investment Limited
Plot No. 1, Block A, Kwa Mrombo Area
Arusha City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of November, 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.


GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 8th day of October, 2024

THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF ARUSHA

........................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name........................................
Signature........................................
Qualification/Relationship
Date........................................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA
*(AT ARUSHA)*

CRIMINAL CASE NO. 25584 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

YUSUF MOHAMED KONDO................................ACCUSED PERSON

To:
Yusuph Mohamed Kondo
Plot No. 92, Block X, Area F
Arusha City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of November, 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 8th day of October, 2024

THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF ARUSHA

........................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name........................................
Signature........................................
Qualification/Relationship
Date........................................

## Serikali yaonya wanaosafirisha wasichana kuwatumikisha kingono

**Na Steven William,** MUHEZA

MGANGA Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Fani Mussa amesema vijiji vingi vya wilaya hiyo kwa sasa vinatishiwa na aina mpya ya ukatili wa usafirishaji wasichana kutoka eneo moja kwenda lingine kwa ajili ya kutumikishwa kingono.

Amesema kuwa kwa mujibu wa takwimu za afya za wilaya hiyo, watu 130 wameripotiwa kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika makundi mbalimbali kwa kipindi cha robo mwaka.

Dk. Fani alifichua hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili kwa watoa huduma za afya kutoka Zahanati na Vituo vya Afya yaliyofanyika katika Hospitali Teule ya Muheza.

"Ukatili wa kijinsia upo aina nyingi. Kwa sasa umeibuka ukatili mpya wa kusafirishwa wasichana kutoka eneo moja kwenda nyingine kwenda kutumikishwa kufanya ngono.

Zaidi alisema, "Ni muhimu jamii kuelekeza nguvu katika mapambano ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kiume, wa kike na wanawake kwa ujumla, kwa kuwa wamekuwa waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili.

"Mkawe mstari wa mbele huko vijijini, kupambana na ukatili wa kijinsia na kutoa elimu kwa wananchi namna ya kupiga vita ukatili, ambao wanaume nao wanapigwa na wake zao lakini hawasemi."

Aidha, aliwatakata watoa huduma hao kutoa takwimu sahihi za ukatili wa kijinsia pale unapotokea katika maeneo yao.

Kwa mujibu wa Dk. Fani, wiki iliyopita alikutana na waganga wa tiba asili na kuwaonya kuacha kujiingiza kuchochea vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema serikali inafikiria kuboresha huduma ya afya kwa wananchi wa wilaya hiyo kwa kuanza kufanya majaribio ya kutoa huduma kwa saa 24 katika zahanati za Kwabada, Nkumba, Magila na Mtindiro.



## HABARI KANDA YA ZIWA

### HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi ambao orodha yao ipo hapa chini waliolipia viwanja kwa nyakati tofauti eneo la Kikombo Kitalu "DA" na "N" kupitia benki, ila taarifa zao zinamapungufu ya majina, namba ya kiwanja na kitalu wafike ya Halmashauri iliyopo Manispaa ya zamani sehemu ya **mauzo ya viwanja** kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao.

Muda wa utekelezaji ni kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2024 hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

Kushindwa kufanya hivyo, umiliki huo hautatambulika tena.

**ORODHA YA MAJINA YENYE TAARIFA PUNGUFU**

| NA | JINA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher Kasung | 10,000.00 |
| 2. | Mbaga Iyombe | 1,000,000.00 |
| 3. | Veisi Maineko | 42,000.00 |
| 4. | George Abel Ngab | 300,000.00 |
| 5. | Ngalawe Hassan Ramadha | 6,931,641.00 |
| 6. | Esther Mpangala | 5,000,000.00 |
| 7. | Victoria Mgala | 400,000.00 |
| 8. | Godfrey K. Msongwe | 9,096,340.00 |
| 9. | Eliaza Mangera Wangwe | 5,148,000.00 |
| 10. | Florence N. Kebwe | 2,515,000.00 |
| 11. | Ali Hussein Habib | 338,300.00 |
| 12. | Joseph Lukumbika | 265,000.00 |
| 13. | Rosina J Delima | 2,249,554.00 |
| 14. | Kelvin Mlambalamba | 1,200,000.00 |
| 15. | Starphod Marwa | 1,000,000.00 |
| 16. | Ally H. Thabit | 3,000,000.00 |
| 17. | Mariam Tawakel | 10,000.00 |
| 18. | Jeremia Baha | 255,000.00 |
| 19. | Shani Mwaruka | 400,000.00 |
| 20. | Ramadhan N Simba | 50,000.00 |
| 21. | Ally Habiba Thabit | 3,000,000.00 |
| 22. | Job Ndalo | 100,000.00 |
| 23. | Giligoli A Ndaro | 100,000.00 |
| 24. | Gloria Reuben Ndaro | 80,000.00 |
| 25. | Magreth W Luma | 10,000.00 |
| 26. | Chedi Ng'enda | 21,729,382.00 |
| 27. | Sospeter N Marco | 2,500,000.00 |
| 28. | Geophrey Mtweve | 1,150,000.00 |
| 29. | Leonary Kimario | 24,000.00 |
| 30. | Lilian Sebastian | 1,625,000.00 |
| 31. | Anna Elisamehe | 400,000.00 |
| 32. | Olais Peter | 300,000.00 |
| 33. | Mussa Deogratius Limb | 4,566,560.00 |
| 34. | Marium | 225,000.00 |
| 35. | Rainer | 4,607,934.00 |
| 36. | George | 100,000.00 |
| 37. | Jafari | 500,000.00 |
| 38. | Dann | 10,000.00 |
| 39. | Victoria | 1,015,000.00 |
| 40. | Jona | 50,000.00 |
| 41. | Alvin | 677,100.00 |
| 423. | Christina | 700,000.00 |
| 43. | Tina | 100,000.00 |
| 44. | Doreen | 300,000.00 |
| 45. | Kelvin | 1,500,000.00 |
| 46. | Innocent | 1,000,000.00 |
| 47. | Mabrouk | 100,000.00 |
| 48. | SHM | 1,000,000.00 |
| 49. | Khadija | 500,000.00 |
| 50. | Jackline | 40,000.00 |
| 51. | Zubeda | 100,000.00 |
| 52. | Kelvin | 250,000.00 |
| 53. | Antony | 180,000.00 |
| 54. | Stanley | 3,500,000.00 |
| 55. | Kelvin | 250,000.00 |
| 56. | | 2,000,000.00 |
| 57 | | 220,000.00 |
| 58. | | 4,447,406.00 |
| 59. | | 2,000,000.00 |
| 60. | | 5,000,000.00 |
| 61. | | 1,566,355.00 |

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**

# Wachimba madini eneo la EACOP

**Na Mohab Dominick**, KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wanaodaiwa kuvamia mgodi wa Maunda kata ya Zongomela Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, linakopita Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Uganda hadi Chongoleani Tanga wamepigwa marufuku na kutakiwa kuacha mara moja shughuli hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kufuatia sintofahamu iliyoibuka baada ya eneo hilo kuvamiwa na kuanza kuchimbwa madini, alisema shughuli yoyote katika eneo hilo ina madhara kwa pande zenye ushirikiano.

"Kama kuna watu tayari wameanza uchimbaji waache mara moja na kama kuna mtu anaona kaonewa basi afuate sheria na taratibu katika kutafuta haki yake," alisema Macha.

Aliendelea kusema kuwa sio lazima watu kufikiria shughuli za uchimbaji bali kuna kazi zingine za kufanya kama vile kilimo ambacho watu wengi wakiwemo vijana wanaonekana kukimbia kufanya kazi hiyo.

"Ni kweli watu walikuwa na leseni katika eneo hilo lakini kuna sehemu bomba la mafuta litapita na kuna watu tayari walishalipwa fidia zao na kama kuna malalamiko basi waende katika mamlaka husika za kisheria kudai haki zao," alisema Macha.

Akizungumza kuhusu hali hiyo, mmiliki wa leseni ya mgodi huo, Asha Msangi alisema tayari amezuia uchimbaji katika baadhi ya maeneo likiwemo hilo linalopitiwa na bomba la mafuta na kuwa kinachoendelea kwa sasa ni watu wameunda magenge ambayo siyo ya wachimbaji.

"Siwezi kuacha watu wakaangamia katika mgodi wangu kwa maafa kwa hiyo ni bora nifunge mgodi waende kulima siwezi kuita polisi kila mara kwa ajili ya kuzuia fujo mgodini kwangu," alisema Msangi.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa kimadini Kahama, Winifrida Mrema alitoa onyo kwa wachimbaji hao na kuwataka wafuate sheria zilizopo kwani eneo lina mipaka yake kwa hiyo hakuna mtu anaruhusiwa kuchimba katika eneo ambalo bomba litapita

# Wajasiriamali wakumbushwa kujirasimisha kuwezeshwa kiuchumi

**Na Benny Kingson,** TABORA

SERIKALI imewataka wajasiriamali nchini kuutumia mpango mpya wa kuwawezesha wananchi kiuchumi IMASA 'Imarisha uchumi na Mama Samia' kwa kujirasimisha kwenye makundi ya wanawake, vijana, wazee na wenye uhitaji maalum, ili kuwezeshwa, kuongeza uzalishaji mali na vipato vyao, jamii na taifa kwa ujumla.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora Dk. Hamisi Kanachi kwenye mkutano wa kuutambulisha mpango huo uliopo chini ya Baraza la uchumi Taifa, NEEC kwa wakazi Tabora.

Dk. Kanachi alisema kuwa endapo wajasiriamali hao watajirasimisha kwenye makundi hayo na kuutumia mpango huo unaoratibiwa nchi nzima pamoja na upande wa pili wa Muungano nchini Zanzibar watakuwa wamesaidiwa kuongeza hali za uzalishaji mali na kuwezeshwa kujipatia vipato zaidi.

**"IMASA imeibua na kuzalisha mikakati ya kimaendeleo kupitia makundi haya, kuyaunganisha na kuwa kitu kimoja, kuwezeshwa, kuzalisha na kupata maendeleo ya uhakika ya familia zenu...**

"IMASA imeibua na kuzalisha mikakati ya kimaendeleo kupitia makundi haya, kuyaunganisha na kuwa kitu kimoja, kuwezeshwa, kuzalisha na kupata maendeleo ya uhakika ya familia zenu, jamii na taifa zima hivyo jamii tuchangamkie fursa kupitia mpango huu,"alisema.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Mhandisi Faustin Tarai alisema kuwa mkoa huo una wakazi milioni 3.3 kati yao wanaume ni milioni 1.6 na wanawake ni milioni 1.7 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 na kwamba wakazi wake wanachangia asilimia 3.9 ya Pato la Taifa.

Alisema halmashauri zake zote zimeweza kutoa mikopo ya Sh. bilioni 12 na milioni 459 ya asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na zimerejeshwa Sh.bilioni 9.99 na pia Sh.bilioni 3.84 zitaongezewa.

Katibu wa Baraza la Uwezeshaji Taifa NEEC, Breng'I Issa alisema programu hiyo ya IMASA itakuwa ni ya miaka mitano na wataanza kwa kutoa elimu kwa walengwa kutoka katika makundi hayo na tunapeleka mpango huu katika mikoa yote 26 ya bara na mitano ya Zanzibar na tutahakikisha tunashuka hadi ngazi ya chini kabisa.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama wamachinga Mkoani Tabora, Zuberi Omari alisema kuwa mpango huo umekuja katika kipindi muafaka na utawakomboa walengwa na anaimani kuwa utashushwa haraka kwenye ngazi za chini ili kuleta tija na ufanisi zaidi.

Nipashe
Spotika



PEP GUARDIOLA, BAADA YA KIPIGO CHA MABAO 2-1 .. UKURASA 13




# GUARDIOLA NA PIGO LA MAJERUHI MAN CITY

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anasema Manchester City ina wachezaji 13 tu ambao ni fiti na wako mashakani baada ya timu yake kuwa na majeruhi zaidi kwenye mechi ya Kombe la Ligi dhidi ya Tottenham Hotspur Jumatano.

City ambao tayari hawakuwa na wachezaji sita wa kikosi cha kwanza kwenye mchezo huo, walimpoteza mlinzi Manuel Akanji kutokana na tatizo la mguu wakati wa maandalizi.

Mshambuliaji Savinho kisha alitolewa nje kwa machela katika dakika ya 63 ya mchezo baada ya kuonekana kuumia kifundo cha mguu.

Guardiola pia alisema beki Ruben Dias, ambaye alitoka mapumzikoni, "anatatizika" wakati mwingine.

"Tuna wachezaji 13 ambao wako fiti, tuko kwenye matatizo makubwa," alisema Guardiola.

"Wanaocheza, wanamaliza wengi wao wakiwa na matatizo na tutaona jinsi wanavyopona.

"Nadhani tuko kwenye shida, kwa sababu katika miaka tisa hatujawahi kuwa katika hali hii ya majeruhi wengi.

"Wachezaji wanapiga hatua mbele, pamoja zaidi kuliko hapo awali, na tutajaribu kufanya hivyo wiki hii katika muda huu mfupi wa kupona."

**Muda wa majeruhi**

Kiungo wa kati na mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or, Rodri atakuwa nje ya uwanja kwa muda wote uliobakia msimu huu baada ya kupasuka mfupa wa mguu Septemba, mwaka huu.

Kiungo mshambuliaji Oscar Bobb pia yuko nje kwa muda mrefu baada ya kuvunjika mguu Agosti. Guardiola alisema wakati huo atakuwa nje kwa miezi mitatu au minne.

Kevin de Bruyne, ambaye alikosa miezi mitano msimu uliopita baada ya kufanyiwa upasuaji, yuko nje kwa sababu ya jeraha la paja na ingawa alitarajiwa kuwa nje kwa muda mfupi tu, Guardiola alisema hivi majuzi kuwa hajui atakaa nje kwa muda gani.

Beki wa pembeni Kyle Walker yuko nje kwa sababu ya jeraha la goti bila tarehe ya kurejea, huku washambuliaji Jeremy Doku na Jack Grealish wakikosa michezo ya hivi majuzi kutokana na majeraha. Guardiola alisema hatarajia, Doku kurudi kabla ya mapumziko ya Kimataifa ya Novemba.

Kabla ya mechi ya Jumatano, Guardiola alikuwa ametaja wachezaji saba pekee wa akiba dhidi ya Southampton wikendi na dhidi ya Sparta Prague wiki iliyopita, huku makipa wawili wakijumuishwa kwenye benchi.

Kwa kuzingatia orodha ya kikosi kwenye tovuti rasmi ya Man City, inaonekana kwamba madai ya Guardiola ni sahihi.

Ni wazi kwamba ataweza kuwaita wachezaji wa timu ya vijana, lakini ukiondoa wale waliojeruhiwa, hawa ni wachezaji wa kikosi cha kwanza wa City wanaopatikana kuwa futi.

**Mabeki**

Nathan Ake, Ruben Dias, Josko Gvardiol, Rico Lewis, John Stones, Josh Wilson-Esbrand

**Viungo**

Phil Foden, Ilkay Gundogan, Mateo Kovacic, James McAtee, Matheus Nunes, Bernardo Silva

**Washambuliaji**

Erling Haaland

Hiyo inaongeza hadi wachezaji 13 wa nje, lakini ni pamoja na Josh Wilson-Esbrand, ambaye hajacheza katika kikosi cha kwanza katika klabu hiyo.

**Athari yake**

Guardiola alisema katika maandalizi ya mchezo huo wa Jumatano tumaini lake kuu lilikuwa kumaliza mchezo huo bila majeraha yoyote.

Ingawa walipoteza kwa Spurs, wachezaji chipukizi katika kikosi cha Man City walionesha matumaini na kuzuia tu Nico O'Reilly mwenye umri wa miaka 19, kufunga bao la dakika za lala salama.

Man City ndio vinara wa Ligi Kuu England, hawajafungwa barani Ulaya, lakini wameshindwa kufuzu kwa robo fainali ya Kombe la Ligi, na Guardiola alisema hivi majuzi ikiwa wachezaji waliojeruhiwa hawatarejea hivi karibuni basi timu yake itajitahidi kushindana katika mashindano mengi.

"Kwa hakika, ikiwa watu hawa hawatarudi haraka iwezekanavyo, tutajitahidi, kwa sababu hatuwezi kuendelea na wachezaji 14, 15 tu kwa msimu," alisema.

"Tunahitaji wachezaji kurejea."

## ISIKUPITE

KIKOSI cha Mikel Arteta, Arsenal, kwa sasa kipo pointi saba nyuma ya vinara Liverpool baada ya mechi kumi, ikumbukwe Blackburn, mwaka 1994, ndiyo timu pekee iliyotoka nyuma zaidi baada ya mechi 10 na kushinda taji la Ligi Kuu England. Walikuwa nyuma ya Newcastle kwa pointi nane, lakini walikuwa wamecheza mechi pungufu kuliko vinara hao. Klabu zingine zilizopata pengo sawa na ambalo Arsenal lazima sasa ilishinde ni Manchester United mnamo 2002-03 na Manchester City msimu wa 2013-14 na 2020-21, huku kila moja ya timu hizo ikiwa nyuma kwa alama sita baada ya mechi 10.






# KAZI NNE ZA AMORIM KUIBADILISHA UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imemteua Ruben Amorim kama kocha mkuu mpya, lakini kocha huyo wa Ureno ana kibarua kizito mikononi mwake ikiwa anataka kubadilisha maisha ya 'Mashetani Wekundu' hao.

United kwa sasa inashika nafasi ya 14 kwenye Ligi Kuu England baada ya kuandikisha ushindi mara tatu pekee kati ya mechi tisa kabla ya mechi ya jana, Jumapili dhidi ya Chelsea.

Ingawa hatutaweza kuona kikosi cha Amorim, United kikiwa uwanjani hadi baada ya mapumziko ya Kimataifa ya Novemba hii, kuna njia chache ambazo bosi huyo wa zamani wa Sporting CP anaweza kuanza kurudisha mafanikio pale Old Trafford.

Hizi hapa kazi nne kwa Ruben Amorim kuibadilisha Man United.

**#1. Kuanzisha utambulisho na mtindo wa kucheza**

Ikiwa Amorim anataka kufanikiwa United, lazima kwanza atekeleze mbinu na mtindo wa uchezaji - mambo mawili ambayo klabu imekuwa ikikosa.

**Historia ya bosi huyo katika uongozi inadhihirisha kwamba haoni shida kuz ielekeza timu zake kucheza anavyotaka, mara nyingi huonesha uwapo wa nguvu kwenye chumba cha kubadilisha nguo.**

Msisitizo wa kumiliki mpira na kuunda muundo, Amorim ameboresha mtindo wa uchezaji pale Sporting unaowaruhusu kutawala michezo na kutishia upinzani.

Baada ya kufungwa mabao mawili pekee katika mechi tisa msimu huu, ni mfumo unaofanya kazi kwa Sporting na unapaswa kuletwa United.

**#2. Kupata timu inayofunga mabao**

Katika mechi tisa za Ligi Kuu England msimu huu, United wamefunga mabao nane pekee. Ili kuweka hilo katika mtazamo, viongozi wa ligi na wapinzani wao, Manchester City wamefunga mabao 20 katika mechi nyingi.

Ni wazi, hili linawakilisha suala kubwa zaidi United, lakini ambalo Amorim anaweza kulitatua.

Kufikia sasa, ni Alejandro Garnacho pekee aliyefunga zaidi ya mara moja msimu huu. Lakini huku Amorim akiwa usukanini, huenda ni wachezaji kama Bruno Fernandes ambao wanafanya vema mbele ya lango.

Ingawa Amorim huwa hachezi na namba 10 wa kawaida, Fernandes anaweza kupewa jukumu jipya kama mshambuliaji wa kati au kuwa mmoja wa viungo wawili wa kati.

Vyovyote vile, timu ikiwa kwenye ukurasa mmoja na huduma zaidi ikitolewa kwa walio mbele, mabao yanapaswa kuja kwa uhuru zaidi.

**#3. Kuondoa wachovu na kuleta wapya**

Katika majira ya joto, United iliangazia wachezaji sita pekee ambao hawakuwa tayari kuachana nao. Iwapo Amorim ana nia ya dhati ya kuwa na matokeo katika klabu, lazima aondoe wasiwasi na kuwakaribisha nyota wenye vipaji anaofikiri watafanya kazi katika mfumo wake.

United ilimsaidia Ten Hag katika madirisha mengi ya uhamisho na kocha huyo wa zamani wa Ajax alileta wachezaji wake wengi wa zamani hapo Manchester msimu uliopita wa majira ya joto.

Ingawa wachezaji hawa waliweza kucheza mechi chache tu chini ya Mholanzi huyo, klabu lazima iwe na imani kamili kwa Amorim, kama alivyofanya Ten Hag, kusajili wachezaji anaowataka katika timu yake.

Mabeki wa kati wenye kasi, viungo wanaocheza mpira - Amorim anajua aina ya wachezaji anaowahitaji na klabu lazima imuamini.

**#4. Kudhibiti kuwa na majeruhi wa mara kwa mara**

Vyanzo vya hivi majuzi vilifichua kwamba Ten Hag mara nyingi alikuwa akiwapa wachezaji wake vipindi vya ziada vya mazoezi kama adhabu kwa kupoteza michezo, jambo ambalo linaweza kuelezea majeraha ya mara kwa mara katika Uwanja wa Old Trafford.

Leny Yoro alikuwa kwenye vitabu vya United kwa si zaidi ya sekunde mbili alipoondolewa kwenye mechi zijazo kutokana na jeraha, Luke Shaw hivi karibuni alikumbana na kikwazo kingine katika safari yake ya kupona jeraha la mguu.

Msimu wa 2023/24, uliangazia madhara makubwa ya majeraha ya United, huku timu hiyo ikikosa pa kugeukia wakati wachezaji hawakupatikana.

Sasa, kazi ya Amorim si kurekebisha majeruhi wa United, lakini ikiwa bosi anaweza kuanza kuzuia wachezaji kutoka kwa uchovu na kuunda timu yenye majukumu na majukumu ya wazi, majeraha yanaweza kuanza kupungua.

## Nukuu

"Bado kuna safari ndefu katika msimu huu, lakini ni safari ndefu sana kwa Arsenal sasa. Arsenal hawakucheza kama mabingwa na sasa wanauguza majeraha yao, wanapaswa kujilaumu tu wenyewe kwa hilo," **Nahodha wa zamani wa Gunners, Martin Keown, baada ya timu hiyo kuchezea kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Newcastle United juzi.**



"Wao [Bournemouth] walikuwa kasi nyingine leo [juzi] na hatukuweza kuimudu. Tulijua hatuwezi kuendana na kiwango. Tulizungumza kuhusu hilo. Ilikuwa ni mchezo wa wazi. Tulipata nafasi mwishoni, lakini naipongeza Bournemouth kwa ushindi huo," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, baada ya kipigo cha mabao 2-1 juzi dhihi ya Bournemouth.**



"Mo Salah maalum, si mara ya kwanza na si mara ya mwisho atafunga kutoka katika nafasi kama hiyo," **Kocha wa Liverpool, Arne Slot, akilizungumzia bao la ushindi la Mohamed Salah wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Brighton juzi.**



# REKODI 5 KALI YANGA IKIPOTEZA KWA AZAM



Nahodha na beki wa kati wa Yanga, Bakari Mwamnyeto (nyuma), akijaribu kumdhibiti straika wa Azam FC, Nassor Saadun, asilete madhara kwenye lango lao, wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa juzi Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, uliomalizika kwa Mabingwa Watetezi, Yanga kuchapwa bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, ilishuhudiwa Yanga ikipoteza kwa bao 1-0.

Yanga imepoteza mechi kwa mara ya kwanza baada ya kushuka dimbani mara nane kwenye Ligi Kuu bila kupoteza msimu huu na kuvunja rekodi iliyoiweka yenyewe msimu uliopita ilipopoteza baada ya michezo mitatu, ikifungwa na Ihefu mabao 2-1, Oktoba 4, mwaka jana katika Uwanja wa Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya.

Ni msimu ambao ilianza kwa kushinda mabao 5-0 dhidi ya KMC, ikashinda tena kwa idadi kama hiyo dhidi ya Tanzania Prisons, kabla ya kukutana na kipigo hicho, ambacho pia kiliweka rekodi ya kuruhusu bao kwa mara ya kwanza kweye Ligi Kuu.

Katika makala haya tunakuletea rekodi tano kali zilizowekwa baada ya mchezo huo kutamatika.

**1# Yanga kupoteza kwa mara ya kwanza**

Hatimaye Yanga imepoteza mechi yake ya kwanza msimu huu baada ya kucheza michezo minane.

Msimu huu ilianza ligi kwa kuifunga Kagera Sugar mabao 2-0, KenGold bao 1-0, ikaifunga KMC 1-0, kabla ya kuitandika Pamba Jiji mabao 4-0, Simba bao 1-0, JKT Tanzania 2-0, Coastal Union 1-0, kisha mchezo wa mwisho kabla ya kupoteza ikashinda 1-0 dhidi ya Singida Black Stars.

**2# Sillah wa kwanza kugusa nyavu za Yanga**

Mchezaji wa Azam raia wa Gambia, Gibril Sillah, amekuwa wa kwanza kugusa nyavu za Yanga ambayo ilikuwa haijaruhusu bao lolote kwa michezo minane iliyopita ya Ligi Kuu.

Bao hilo la dakika ya 32, mbali na kuweka rekodi ya kuwa mchezo wa kwanza kufunga bao kwenye lango la Yanga, pia imeipa Azam ushindi wa bao 1-0 na kuchukua pointi tatu kwenye mchezo huo.

**3# Mara ya mwisho Yanga ilifungwa na Azam**

Ni kama Azam FC ilianzia ilipoishia kwani mara ya mwisho zilipokutana, Machi 17, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu uliopita, ilishinda mabao 2-1.

Yanga mara ya mwisho ilifungwa mabao hayo dhidi ya Azam, na imelinda rekodi ya kutopoteza kwenye Ligi Kuu mpaka pale ilipokipiga tena kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza msimu huu na kuchapwa bao 1-0

**4# Sillah anajua siri ya Diarra?**

Hii ni mara ya tatu kwa winga wa Azam, Sillah kumtungua kipa wa Yanga, Djigui Diarra raia wa Mali, katika michezo yote ambayo timu hizo zimekutana.

Juzi alifunga akimtungua Diarra dakika ya 32 na kuipa Azam ushindi wa bao 1-0, lakini pia alimfunga dakika ya 19 katika mchezo wa mzunguko wa pili msimu uliopita uliochezwa Machi 17, mwaka huu, Azam ikiifunga Yanga mabao 2-1, akisawazisha bao la dakika ya 10 la Clement Mzize kabla ya Feisal Salum kufunga la ushindi dakika ya 51.

Sillah, ambaye alisajiliwa na Azam, 2023 akitokea Klabu ya Raja Casablanca ya Morocco, alimfunga kipa huyo katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu msimu uliopita, uliochezwa Oktoba 23, mwaka jana, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, japo Azam ilifungwa mabao 3-2, yote yakifungwa na Stephane Aziz Ki, lakini Sillah alimtungua Diarra dakika ya 19, na lingine likifungwa na Prince Dube kwa mkwaju wa penalti kabla ya kuhamia Yanga msimu huu.


**5# Yanga imepoteza nyumbani**

Yanga imeungana na timu za Simba, Azam na Singida Black Stars si kupoteza mechi moja tu, bali kupoteza uwanja wa nyumbani.

Mechi moja moja ambazo timu hizo zimepoteza, zilicheza kwenye viwanja vyao vya nyumbani. Yanga iliutumia Uwanja wa Azam Complex juzi kama wake wa nyumbani, ikafungwa kwa mara ya kwanza dhidi ya Azam bao 1-0, ikiungana na Singida Black Stars ambayo ilifungwa kwa mara ya kwanza Oktoba 30, mwaka huu, ikiutumia Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar kama wake wa nyumbani dhidi ya Yanga, ikachapwa bao 1-0.

Azam, nayo iliutumia uwanja huo kuwa wa nyumbani ilipocheza dhidi ya Simba, Septemba 26 na kutandikwa mabao 2-0, huku Simba nayo ilifungwa bao 1-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Yanga, mchezo ambao kikanuni ilikuwa ni mwenyeji.

**JE, WAJUA?**



KABLA ya kipigo cha Jumamosi dhidi ya Bournemouth, mechi ya mwisho kwa Manchester City kupoteza ilikuwa dhidi ya Aston Villa Desemba 6, mwaka jana. Katika kipindi hicho ilishinda mechi 26 na sare sita, huku ikifunga mabao 80 na kuruhusu 26 tu, hivyo kuvuna alama 84 zilizoiwezesha kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu wa 2023-24, ikiwa ni kwa mara ya nne mfululizo.



# Madiwani wajivunia kukusanya bil. 1.3/-

**Na Mwandishi Wetu,** ITIGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Itigi, mkoani Singida, imefanikiwa kukusanya takribani Sh. bilioni 1.3 sawa na asilimia 50 katika robo ya kwanza ya mwaka katika kipindi cha mwezi Julai na Septemba 2024.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hussein Simba, akizungumza juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani, alisema mafanikio katika ukusanyaji huo yametokana na ushirikiano uliopo baina ya madiwani na watumishi.

Simba aliwataka watumishi wa halmashauri hiyo kuendelea kujenga ushirikiano na upendo, ili kuleta ufanisi katika ukusanyaji mapato na usimamizi wa miradi.

Alisema mahali popote pale hakuwezi kuwa na mafanikio kama hakuna ushirikiano,upendo na mashauriano.

"Kufinyana kupo kwa yule ambaye haendani na sisi lakini kwa yule anayesikia tutaenda naye maana huwezi kuwa na watoto wote wanakuitia ndio lazima awepo mtukutu, nakupongeza Mkurugenzi na watumishi wako mambo yanakwenda vizuri sana," alisema.

Simba aliwataka madiwani na watendaji kuhakikisha wanasimamia miradi ya maendeleo ambayo serikali imetoa fedha, ili iweze kujengwa vizuri kulingana na thamani ya fedha.

"Hivi sasa tumeletewa Sh.milioni 544 kujenga shule mpya zamani tulikuwa tunachangishana na hatufikii malengo ya kujenga, lakini hivi sasa serikali inatuletea mamilioni kutekeleza miradi jukumu letu kubwa ni kuisimamia," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk.Vicent Mashinji, alisisitiza umuhimu wa ukusanyaji mapato kwa halmashauri na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

# Waandishi 316 wapata madhila kazini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAANDISHI wa habari 316 wamepata madhila nchini, yakiwamo ya kukamatwa, vitisho, kutekwa na watu wasiojulikana katika kipindi cha kuanzia 2012 hadi Oktoba 2024.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura, aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili dhidi ya Waandishi wa Habari (IDEI) yaliyofanyika mkoani Singida.

Alisema kuwa katika kipindi hicho wamekamatwa waandishi 31, waliopewa vitisho walikuwa wanane huku matukio mengine na idadi kwenye mabano ni kutekwa (1), onyo kwa vyombo vya habari (4), vyombo cha habari kufungiwa (4), kipindi kukatishwa kikiwa hewani (1) na kunyimwa taarifa (1).

Madhila mengine waliyopata waandishi wa habari ni uhuru wa mahakama kuingiliwa (1) na kunyang'anywa vifaa (1) na kwamba kati ya hao wanaume ni 36 na wanawake ni wanane.

Sungura ambaye pia ni Mwenyekiti wa Muungano wa Haki ya Taarifa (CoRI) na Mtandao wa Mabaraza Huru ya Habari Afrika, alisema kwa mujibu wa taarifa ya ufuatiliaji za Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), ukatili dhidi ya waandishi wa habari ni mkubwa.

Alisema mwaka 2022, madhila 19 yalirekodiwa, 2023 madhila 23 na mwaka huu 2024 hadi kufikia Oktoba yamerekodiwa madhila 33.

Alisema kati ya 2006 hadi 2024, zaidi ya waandishi 1,700 wameuawa duniani na kesi za mauaji hayo asilimia 90 hazijatatuliwa mahakamani.

"Serikali ya Tanzania ina kila sababu ya kuongeza nguvu ya kuwalinda waandishi wa habari dhidi ya madhila kufuatia kuongezeka kwa madhila dhidi yao kwa mwaka huu 2024 kulinganisha na miaka miwili iliyopita " alisema.

> **"Kwa upande mwingine chini ya uratibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni hatua muhimu katika kuchechemua mazingira wezeshi na salama ...**

Sungura alisema CoRI inaunga mkono mazungumzo kati ya serikali na wadau wa habari katika kujenga mwafaka na kukubaliana na ukatili dhidi ya waandishi wa habari hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu utakaofanyika 2025.

Aliongeza kuwa ripoti ya Taasisi ya Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka (RSF) inaonesha Tanzania imepanda katika viwango vya uhuru wa habari kutoka nafasi 143 mwaka jana hadi kufikia nafasi ya 98 mwaka huu.

"Taarifa kwamba wiki ijayo Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa upande mmoja wanakutana na baadhi ya wadau wa CoRI.

"Kwa upande mwingine chini ya uratibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni hatua muhimu katika kuchechemua mazingira wezeshi na salama kwa waandishi wa habari kutekeleza wajibu wao wa msingi wa kupashahabari,kufichua uovu na kuelimishaumma kwa uhuru ili kulijenga taifa la Tanzaniakidemokrasia," alisema.

Alisema NIMCA na CoRI yanapinga ukatili dhidi ya waandishi wa habari na kuunga mkono juhudi za kila serikali duniani katika kuzungumza na wadau wa habari, ili kuweka mazingira wezeshi ya kuwalinda waandishi wa habari kwa gharama zozote.

Mkurugenzi wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Kenneth Simbaya alisema umoja huo umewapa mafunzo waratibu kwenye klabu za waandishi kila mkoa ambao ndio wanakusanya takwimu za madhila wanayopata waandishi wa habari.

Alisema UTPC baada ya kupata taarifa kitengo cha ulinzi na usalama huwa zinajadiwa na kuchukua hatua ya namna ya kuwasaidia waandishi wa habari waliopata madhila kwa kuwapatia msaada wa kisheria.



Rais wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Deogratius Nsokolo, akizungumza jana wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa UTPC unaofanyika mjini Singida na kuwashirikisha wenyeviti, makatibu na waweka hazina wa klabu za waandishi wa habari kutoka mikoa 28 ya Tanzania Bara na Zanzibar. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TLS kujadili mchakato wa Katiba mpya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUTANO maalumu wa kitaaluma wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali, ukiwamo mchakato wa Katiba mpya, umepangwa kufanyika Novemba 11 hadi 16 jijini Arusha.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Rais wa TLS, Boniface Mwambukusi, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano uliofanyika jijini Dodoma.

Alisema katika mkutano huo watajadili suala la mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya,ikiwemo kuangalia wapi tulipotoka na tunaelekea wapi.

Alisema lengo lao TLS katika mjadala utakaolenga suala la mchakato wa Katiba mpya kupata ambayo itaendana na hali ya sasa ya kimaendeleo.

"Katika majadiliano yetu, suala hilo pia litapewa kipaumbele kujadiliwa ikiwemo kutoa maoni na mapendekezo yao,"alisema Mwabukusi.

Kutokana na hilo, alitoa wito kwa mawakili wote pamoja na wanataaluma hiyo,wakiwemo wanachama wa TLS kushiriki mkutano huo uliopangwa kufanyika Arusha.

Mbali na hilo, Mwabukusi alisema katika mkutano huo watajadili suala la utunzaji data katika mambo mbalimbali wanayofanya kwenye taaluma hiyo.

Alisema suala la utunzaji data ni muhimu hivyo litapewa kipaumbele katika mkutano unaoshirikisha mawakili na wanataaluma kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mwabukusi alisema ukiacha suala zima la utunzaji data, watapokea maoni kutoka kwa washiriki wa mkutano huo ya namna ya uwajibikaji wa TLS katika maeneo mbalimbali,ikiwemo mchakato wa upatikanaji Kaatiba mpya.

"Tutapokea maoni kuhusu uwajibikaji wa TLS,kwenye majukumu ya mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya,tunahitaji kupata Katiba itakayoendana na hali ya sasa,naamini washiriki wa mkutano huo watapata fursa ya kutoa mapendekezo yao," alisema Mwabukusi.

Katika hatua nyingine, Mwabukusi alisisitiza jamii ijitokeze kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa,kwa sababu ni haki ya kila mmoja kushiriki.

Alisema hakuna sababu ya kuhofia kitu chochote,kinachotakiwa ni kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuchagua viongozi katika nafasi mbalimbali.

Aidha, alivitaka vyama vya siasa kutenda haki kwa wagombea watakaopata nafasi ya kugombea katika nafasi mbalimbali ambazo watawania.





# TEHAMA kutumika kufundisha sayansi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya TEHAMA pamoja na taasisi ya QSOFT Technology zimeanza mchakato wa kufunga mfumo wa TEHAMA kwa baadhi ya shule za sekondari mkoani humo.

Aidha, mfumo huo ni kwa ajili ya kufundishia huku lengo likiwa ni kukabiliana na tatizo la uhaba wa walimu ikiwemo wa masomo ya Sayansi

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki katika kikao cha mwisho wa mwezi cha Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka na watumishi wa mkoa huo, taasisi za kiserikali, wakuu wa wilaya, wakurugenzi na kamati ya ulinzi na usalama kilichofanyika ofisini kwake.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya TEHAMA, Prof. Leonard Mselle alisema serikali imedhamiria kufanya mageuzi kitaaluma kupitia teknolojia hivyo wanakwenda kushirikiana kufunga mifumo ambayo itatumika kufundishia madarasa mengi kwa wakati mmoja hatua ambayo itakuwa suluhisho la upungufu wa walimu.

> **Awali Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mtaka alisema ni jambo la kushangaza kuona bado kuna vilio vya uhaba wa walimu nchini wakati kuna maendeleo makubwa ya teknolojia, hivyo kila mkurugenzi mkoani humo**

"Tunaposema matumizi ya tehama yatumike tunataka mtu wa chini kabisa atumie tehama na sio usanii usanii tu, mtoto wa masikini Tanzania kijijini huko atumie tehama kusoma, atumie tehama kama mtoto wa nchini China na kwengineko," alisema Mselle.

Naye Mhandisi Amili Bahanza kutoka Kampuni Teknolojia ya QSOFT alisema wazo hilo limekuja ili kuona namna gani shule za kawaida zinaweza kufikiwa katika upande wa tehama.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mtaka alisema ni jambo la kushangaza kuona bado kuna vilio vya uhaba wa walimu nchini wakati kuna maendeleo makubwa ya teknolojia, hivyo kila mkurugenzi mkoani humo ajipange kuanza na shule chache za sekondari kufunga mifumo ya tehama ili itumike kufundisha wanafunzi.

"Ningekuwa mkurugenzi ningweka mfano, siwezi kuwa mkurugenzi nina kata sita nikaandika barua Tamisemi kwamba nina uoungufu wa walimu wa sayansi wakati nina tehama kwenye kata zangu tisa, nina umeme ningekuwa mkurugenzi wa kwanza ambaye nina halmashauri ambayo inafundisha kwa TEHAMA," alisema Mtaka.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe alisema licha ya mkoa kujipambanua kuanza matumizi ya TEHAMA kufundisha, lakini ili kufikia malengo wanakwenda kutenga bajeti ya kutekeleza mpango huo ili kuwa mkoa wa mfano nchini kwa matumizi ya tehama kwenye elimu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Gracian Makota (kulia), akimkabidhi tuzo mmoja wa wakurugenzi wenza wa kampuni, Damas Mwakipesile, kutambua mchango wao kusaidia jamii inayozunguka migodi ya madini ya Tanzanite, mji mdogo wa Mirerani mwishoni mwa wiki. **PICHA: GIFT THADEY**

# H'mashauri kuwasaka wanaokiuka taratibu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Njombe mkoani Njombe, imetangaza kuwasaka na kuwachukulia hatua kali za kisheria wafanyabiashara wa mazao, madalali na watendaji ambao wanakiuka taratibu za utumishi wa umma kwa kuamua kushirikiana na wafanyabiashara wasio waaminifu kutorosha mapato.

Mapato yanayodaiwa kutoroshwa yanatokana na mazao ya viazi, mbao, parachichi, maharage na chai kwa kutumia barabara ambazo sio rasmi na kuisababishia hasara na makusanyo machache ya mapato ya halmashauri.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025 kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo Lunyanywi.

Baadhi ya madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Njombe akiwemo Geofrey Mhando alisema kuna wafanyabiashara wananunua mazao halmashauri ya mji wa Njombe na kisha kwenda kukata ushuru Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa. "Pia kuna soko la mbao uwemba nalo linachangia upotevu mkubwa wa mapato ya serikali na hatua za haraka zinazopaswa kuchukuliwa ili kunusuru hali hii kwa sababu tunakosa mapato," alisema Mhando.

Naye Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Njombe Mjini, Tumaini Mtewa aliomba kufuatiliwa kwa ushuru katika soko la wakulima kwa sababu eneo hilo kila siku mizigo inashushwa. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete alisema vyanzo vyote viliyotajwa kupoteza mapato vinakwenda vinachunguzwa na kisha kutaka watendaji na wafanyabiashara kuwa wazalendo kwa taifa lao.

Akiwasilisha salamu za serikali kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe Kissa Kasongwa, Ofisa Tarafa Njombe mjini Lilian Nyemele aliwahimiza madiwani kuhakikisha wanaendelea kusimamia kwa ubora miradi inayoanza pamoja na ile ambayo haijakamilika (miradi viporo) ili iweze kukamilika na kuanza kuwahudumia wananchi.

Alisema msimu wa kilimo unakaribia, hivyo ni jukumu la viongozi na wakulima wote kuhakikisha shughuli za kilimo zinafanyika kwa ufanisi na endapo tatizo likijitokeza ni vema taarifa ikatolewa mapema ili kuongeza uzalishaji na kuhimarisha usalama wa chakula.

# Wazalishaji bidhaa watakiwa kuzingatia viwango vya TBS

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

WAZALISHAJI nchini wametakiwa kuhakikisha bidhaa wanazozalisha zina alama ya ubora inayotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ili kuziwezesha kupelekwa nje ya nchi ikiwemo kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) bila vikwazo vyovyote.

Hatua ni kutokana na nchi za EAC kuwa na makubaliano, ambapo bidhaa ikishathibitishwa ubora na shirika la viwango la nchi husika na kupata alama ya ubora haitakiwi kupimwa tena ndani ya nchi za jumuiya hiyo.

Rai hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Meneja wa TBS Kanda ya Kati, Hamis Seleleko wakati akizungumza na wananchi, wazalishaji, wafanyabiashara na wawekezaji kwenye Maonesho ya Maadhimisho ya Tatu ya Wiki ya Mwanakatavi yaliyofanyika mjini Mpanda kuanzia Oktoba 25 hadi 31 mwaka huu.

Alisema lengo la kushiriki kwenye maonesho hayo ni kutoa elimu ya huduma ambazo zinatolewa na TBS ikiwemo utoaji alama ya ubora kwa bidhaa ambazo zinazalishwa nchini, ili kujiridhisha na ubora wake na kuziongeza thamani ili ziweze kukubalika kwa walaji.

"Lakini pia ni kuziwezesha kupelekwa nje kwa mfano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki bidhaa ambayo itakuwa imepata alama ya ubora itapelekwa nchi yoyote bila ya kuwa na vikwazo vya kibiashara," alisisitiza Seleleko.

Aidha, alisema sambamba na hilo wameshiriki maonesho hayo kuwaeleza wananchi kuwa wanatoa huduma ya vipimo kwa kupima bidhaa mbalimbali katika maabara za shirika hilo zilizopo Dar es Salaam.

Seleleko alisema maabara hizo zina ithibati, hivyo zinatambuliwa kimataifa na bidhaa yoyote ikishapimwa kwenye maabara hizo inakuwa inatambulika kimataifa, haitakiwi kupimwa tena.

"Kwa hiyo kupitia kwenye maonesho haya tumewasihi kuwa bidhaa zinazotakiwa kuingia sokoni zile zinazokidhi matakwa ya viwango husika," alisema.

Meneja huyo pia alitaja matatizo ambayo wanaweza kukumbana nazo kwa kuuza bidhaa ambazo hazikidhi matakwa ya viwango kuwa ni pamoja na kuziondoa sokoni zikiwemo bidhaa zilizopigwa marufuku kwenye soko la Tanzania vikiwemo vipodozi vyenye viambata sumu.

"Kwa hiyo tunawaambia wananchi, wafanyabiashara na wajasiriamali wazingatie viwango vilivyowekwa na serikali kupitia TBS," alisema Seleleko.

Lengo la maonesho hayo ni kutangaza fursa za kiuchumi za Mkoa wa Katavi na fursa hizo ikiwa ni pamoja na uwekezaji, kilimo, madini, utalii na ufugaji.



# Usafirishaji vifurushi kimataifa waongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya Hali ya Mawasiliano kufikia Septemba mwaka huu inaonesha idadi ya vitu vinavyosafirishwa kutoka Tanzania kwenda kimataifa na mtoa huduma wa Posta Kitaifa, imeongezeka kufikia asilimia 74.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ambayo ilitolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), idadi hiyo ilishuka mwaka 2019 hadi 2021.

Taarifa ya robo mwaka ya Julai hadi Septemba 2024 inaonesha kuwa vitu vilivyosafirishwa na Shirika la Posta Tanzania (TPC) kwenda nje ya nchi viliongezeka kwa asilimia 74 kati ya mwaka 2021 na 2023.

Taarifa inasema vitu 979,625 vilipostiwa kimataifa mwaka 2023 kulinganishwa na vitu 564,528 mwaka 2021, mwaka uliooshuhudia kuanza kuongezeka kwa vitu kwenda nje baada ya kupungua miaka iliyotangulia.

"Vitu 2,873,312 vilisafirishwa kimataifa mwaka 2019. Idadi hiyo ilipungua na kufikia 564,528 mwaka 2021. Sekta ya posta ulimwenguni kote imekumbwa na changamoto zinazotokana na kuenea kwa kasi kwa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)," ilibainisha ripoti hiyo.

Akifafanua kuhusu ripoti hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, alisema kuwa hali hiyo iliwapa watumiaji huduma za posta mbadala wa mawasiliano, mawasiliano ya kielektroniki yakiongeza ufanisi kwenye shughuli za watumiaji.

Alisema janga la UVIKO 19 pia limechangia kuzorota kwa huduma za posta kutokana na kuvurugika kwa mifumo ya usafirishaji vitu vya posta.

Hata hivyo, alisema watoa huduma wa posta wanatumia TEHAMA kwenye shughuli zao na wengine wameanzisha huduma mbadala. "TCRA inahimiza watoa huduma wa posta na vifurushi kutumia teknolojia za kisasa zenye ufanisi. Hizi ni pamoja na mifumo ya kidijiti na mifumo inayojiendesha yenyewe ambayo hurahisisha utendaji na kuboresha upatikanaji wa huduma za posta," alisema.

TCRA imetoa leseni 146 kwa watoa huduma za posta na usafirishaji vifurushi, ambazo ziko kwenye makundi sita ambayo pia ni aina ya soko la huduma husika.

Makundi ya watoa huduma za usafirishaji vifurushi, na idadi ya leseni kwenye mabano ni; kimataifa (6), Afrika Mashariki (2), ndani ya Tanzania (47), ndani ya mji au jiji (16) na kati ya miji (74). Leseni nyingi za kati ya miji zimetolewa kwa wasafirishaji, yakiwamo mabasi ya abiria. Alisema TCRA inafanya ukaguzi kila robo mwaka kutathmini uzingatiaji kanuni za leseni na ubora wa huduma na kwamba vipimo ni pamoja na kuzingatia kasi ya kufikisha vitu vinavyotumwa na wateja. Tathmini ya robo mwaka ya Julai-Septemba ilihusisha watoa huduma 19 imegundua kuwa watoa huduma saba, au asilimia 37, tu ndio waliofikisha vitu kwa wakati uliowekwa kikanuni.

Kampuni zilizozingatia matakwa ya kanuni ni Air Tanzania, Precision Air, Tanz Movers, Advanced Logistics, Delex Courier & Logistics Limited, Ellymo Company Limited na Segax.

Kampuni 12 hazikukidhi mahitaji ya kanuni za ubora wa huduma.

# Wanaofanya uvuvi haramu waonywa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Hifadhi ya Bahari Tumbatu (TUMCA), Yassir Ali Haji amewataka wavuvi kuachana na uvuvi haramu na kutumia mitego inayokubalika kisheria kwa lengo la kuimarisha bahari na rasilimali zake.

Aliyasema hayo jana Mkokotoni, mkoa wa Kaskazini Unguja wakati wa doria shirikishi katika hifadhi hiyo.

Alisema mitego inayokubalika kisheria katika hifadhi za bahari ni nyavu zenye ukubwa wa nchi tatu na madema ya miti pamoja na mishipi, ili kulinda matumbawe pamoja na mazalia ya samaki baharini.

Alisema idara imeamua kufanya doria za kuvikamata vyombo vyote vyenye kujihusisha na nyezo zisizokubalika kisheria jambo, ambalo hupelekea kupungua kwa uzalishaji wa samaki kwa wingi.

Katibu wa Ulinzi Shiriki ya CMG ya Mafundani, Mustafa Shazil aliwataka wavuvi kuachana na mitego isiyokubalika kisheria kwa lengo la kuimarisha mazingira ya bahari kwa maslahi ya sasa na baadaye.

**Wakizungumza katika zoezi hilo, baadhi ya wavuvi walisema wapo tayari kuachana na uvuvi haramu kutokana na hasara walizozipata baada ya kukamatwa kwa vyombo vyao jambo ambalo ...**

Wakizungumza katika zoezi hilo, baadhi ya wavuvi walisema wapo tayari kuachana na uvuvi haramu kutokana na hasara walizozipata baada ya kukamatwa kwa vyombo vyao jambo ambalo limerejesha nyuma hali zao za kiuchumi.

Zoezi hilo limefanyika na idara ya uhifadhi wa bahari kwa kushirikiana na Kikosi cha KMKM polisi utalii, diplomasia na kamati za uvuvi.

Zaidi ya vyombo 10 vimekamatwa vikiwa na dhana haramu na kutolewa hukumu nje ya mahakama na kutozwa faini ya Sh. 100,000 kwa kila chombo na huku wahusika wamejaza mikataba ya kutorejea tena makosa hayo.



Mgeni rasmi kwenye mahafali ya wanafunzi wa Shule ya Montissori ya Mangapwani, mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkurugenzi wa Elimu Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mussa Said (kulia) akipata maelezo ya ujenzi wa madarasa kutoka kwa Mkuu wa Shule hiyo, Susan Maziku (wa pili kushoto). **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Tamasha la Trace Awards kuongeza utalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUFANYIKA kwa tamasha la muziki wa tuzo ya Trace Awards, visiwani Zanzibar kutasaidia kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea visiwa hivyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari huko Matemwe, mkoa wa Kaskazini Unguja, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhani Soraga alisema tamasha hilo ni chachu ya kuongeza pato la nchi.

Alisema kuwa tamasha hilo lina umuhimu mkubwa kufanyika ambalo litawashirikisha watu mashuhuri na wasanii mbalimbali wanaotamba hivi sasa.

Waziri Soraga alisema kuwa Trace Award ni kama kampuni ya mawasiliano na mashabiki wengi wakifuatilia taasisi hiyo hivyo kuwepo Zanzibar inakwenda kuonesha ramani ya dunia kuwa Zanzibar ina visiwa vizuri kwa shughuli ya utalii.

"Hivi sasa Trace Awards imekuwa maarufu sana na kuwa na mashabiki wengi wakiifuatia Zanzibar ni bahati ya pekee kuja kwa tamasha hilo sisi visiwa vya utalii lazima tuonekane " alisema Waziri Soraga.

Aidha, alisema kuwa serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya malazi kwa wageni wanaotarajiwa kufika ili kuendelea kuipa heshima Zanzibar katika mataifa mengine mbalimbali.

Alisema kuwa imejipanga katika kuhakikisha kuwa utalii unaendelea kukuwa hasa kubuniwa kuleta matamasha ,mikutano ya kimataifa, ili wageni kuona uzuri wa kisiwa cha Zanzibar .

"Sisi tumeamua kuja na ubunifu na katika kuitangaza Zanzibar kiutalii kwa kutangaza fursa za kufanyika mikutano na matamasha," alisema Soraga.

Meneja wa Hoteli ya The More Reda Sweed Zanzibar, alisema kuwapo tuzo hizo kutasaidia kuongeza idadi ya watalii pamoja na wawekezaji wanaokuja kuwekeza kisiwa cha Zanzibar.

Alifahamisha kuwa wao kama wawekezaji wa mahoteli wamejipanga katika kuwapokea wageni watakao kuja hapa Zanzibar.

"Uhalisia sisi kama wawekezaji tumejipanga kuwapokea wageni wa tamasha hilo na Zanzibar ni nchi ya amani zaidi duniani," alisema. Mkurugenzi Mzalishaji wa Trace Awards, Seven Moshi aliesema lengo la tunzo hiyo ni kuutangaza muziki wa kizazi kipya Tanzania kujilikana kimataifa.

Alisema mbali ya kuwafanya waimbaji wa Tanzania kujulikana pia itakuwa nafasi adhimu kwa Zanzibar kutangaza fursa ya utalii na kuongeza namba ya wawekeji.

Tamasha hilo linatarajiwa kufanyika Februari 24 hadi 26 mwakani visiwani humo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHELIMOO CLEMENT CHIME** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1522/0006** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SCOLASTICA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/235436/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DOREEN PRISCUSS LUCAS**

Anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S 0485/0034** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Majengo mwaka 2017. Kwa yeyote atakaye kiona atoe, Taarifa kituo chochote cha polisi **PHQ/ KIL/MS/26507/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SUSAN ALPHONCE KOLIMBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha Diploma ya Ualimu, chenye index namba **506/012** kilichotolewa kupitia **MARANGU TEACHERS COLLEGE.** Mwaka 1988. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN//238380/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PASENCE PASCHAL KABANGO** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne, chenye index namba **S.4631/0062/2015** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KAIZIREGE SECONDARY SCHOOL.** Mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/KAG/BUK//15763/2024.**

## TANGAZO LA KAZI/UALIMU

Tunatangaza nafasi za kazi ya ualimu mchepuo wa kingereza kwa masomo yote na madarasa yote kuanzia chekechea Hadi darasa la saba, sifa za chekechea ni certicate au diploma na kwa darasa la kwanza Hadi la saba ni diploma au shahada ya kwanza ya elimu.

**Mawasiliano 0783298900**

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COIRT SUB-REGUSTRT**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTER)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.124 OF 2024.**

**IN THE MATTER OF THE PROBATE AND ADMINISTRATION OF ESTATES ACT {CAP 352 2002}**

**IN THE MATTER OF ADMINISTRATION OF ESTATE OF THE LATE JAYANTILAL NAGINDAS MEISURIA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF PROBATE OF BY SHAILESH KABTULAL MEISURIA AND MAYUR KANTILAL MEISURIA WITH WILL ANNEXED.**

**NOTICE TO CREDITORS**

**(Made under rule 111 of the Probate and Administration of Estate Rules, Cap 35 2 R: E2002)**

**NOTICE TO CREDITORS**
**(Rule 111)**

**NOTICE** is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the **LATE JAYANTILAL NAGINDAS MEISURIA** the above-named deceased, who died at **LONDON HEALTH CENTER** On the 22ND day of JULY 2024 and probate of whose will and letter of administrations were granted to **SHAILESH KANTILAL MEISURIA** and **MAYUR KANTILAL MEISURIA** by the Court on the 29th day of October 2024, are hereby required to send in their claims to us at the address appearing on the letterhead within SEVEN DAYS from the date of the publication of this notice at the expiration of which time WE shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims of which WE shall then have had notice.

...............................................
*SHAILESH KANTILAL MEISURIA -Executor Executor*

...............................................
*MAYUR KANTILAL MEISURIA-*

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.26912 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MICHAEL WALUSE JOSEPH————————DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**

**1. CAREN ELIAKIM GIBANGA————————PETITIONER**
**2. PHILBERT RIANA WALUSE............. PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 13th day of NOVEMBER,2024.

Dated at Morogoro this 28TH day of OCTOBER 2024.

.....................................
***PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE***
**MOROGORO DISTRICT COURT**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
MOROGORO

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.26772 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**

**ALOYCE JACOB MATAHIMBA—————————DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**

**1. MICHAEL ALOYCE MATAHIMBA——————PETITIONER**
**2............................................**

**GENERAL CITATION**
**(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 07th day of NOVEMBER,2024.
Dated at Morogoro this 28TH day of OCTOBER 2024.

.....................................
***PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE***
**MOROGORO DISTRICT COURT**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
MOROGORO

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and administration Cause No 26171 of 2024**

**In the Matter of the estate of the late FRANICS SEVERIN CHAILA of Mlimwa C within Dodoma Region**

**And**

**In the matter of Application for letters of Administration by BETHANIA FRANCIS CHAILA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of November...................... 2024
Dated at Dodoma this 29th day of October......................2024

.....................................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA RESIDENT MAGISTRATE'S COURT

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26336 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HAPPYNES SAMWEL CHALLANGE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PAULO DASTAN MNGUMI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21st day of NOVEMBER 2024.
Dated at KOROGWE this 21st day of OCTOBER, 2024.

.....................................
**RESIDENT MAGISTRATE**
**KOROGWE**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Bosi Dar24 afunguka sababu za kupotea

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI wa Dar24, Maclean Mwaijonga, ameibuka na kusimulia sababu za kutoonekana akidai "kufanyiziwa" na wafanyabiashara wenzake.

Amedaiwa kuwa baada ya kutoka kazini Oktoba 31 mwaka huu, kuna wafanyabiashara alipanga kukutana nao Kigamboni kwa ajili ya kuzungumza masuala ya kibiashara.

Ameeleza kuwa aliendesha gari hadi Kigamboni na kitu anachokikumbuka cha mwisho ni kwamba aliagiza juisi na baada ya kuinywa alianza kujisikia kizunguzungu na dakika chache baadaye alipoteza fahamu.

Mwaijonga aliyabainisha hayo usiku wa kuamkia jana katika mazungumzo na ITV muda mfupi baada ya kuonekana, akidai kuwa kilichotokea baada ya hapo hakikumbuki.

Alidai kuwa baada ya kupata fahamu, kuna watu waliokuwa wanamwuliza maswali kuhusu taarifa zaidi za biashara anazozifanya.

Oktoba 31 mwaka huu, majira ya alasiri kulisambazwa taarifa katika mitandao ya kijamii kuhusu kutoweka kwa Mwaijonga, hali iliyolifanya Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam juzi kutoa taarifa kuwa linamtafuta mfanyabiashara huyo.

"Waliuliza pia kuhusu nywila zangu na baada ya kuona wameshindwa walinipakia katika gari wakanizungusha sehemu ambazo sizifahamu lakini mwisho wa siku wakaniacha. Nisisitize kwamba ni watu ambao ninawafahamu, tulikuwa tunaongea biashara, sikutegemea kitu kama hicho kingetokea.

"Kwenye gari tulikuwa wote wakati wananizungusha, nilikuwa siko sawa lakini nilikuwa ninawaona sura zao na wakanishusha maeneo ya Buyuni, Kigamboni. Nilipoona wameniacha pale kama wamenitelekeza, nahisi ni baada ya kuona hawajafanikiwa kupata walichokitaka, nikawa ninatafuta mtu wa kunisaidia mawasiliano.

"Nilivyopata simu nikampigia mzee wangu ambaye ninafanya naye kazi kwa muda mrefu, akafika pale na polisi wakanichukua na kunipitisha hospitalini kuangalia hali yangu, sasa hivi ninaendelea vizuri," alisimulia Mwaijonga.

Aliendelea kusimulia kuwa kitu kilichosababisha aende kukutana na watu hao ni kwamba walikuwa na wazo la kibiashara walilotaka washirikiane, akieleza kuwa walimwalika ili wakafanye maongezi ndipo mkasa huo ulikoanzia.

"Ninachoweza kuwaambia watu hawa ni watu ambao ninawafahamu vizuri lakini ni kwa sababu walikuwa na nia ovu, lakini imeshindikana, na ninashukuru Mungu mimi ni mzima wa afya, nia yao imeshindikana walikuwa labda wanataka kupata taarifa za biashara ninazofanya," alisema Mwaijonga.

Alishukuru Jeshi la Polisi kwa kufika eneo la tukio mapema, akieleza kuwa mkasa huo unahusiana na masuala ya kibiashara na watu waliokuwa na nia ovu na si mambo ya uandishi wa habari.

Mwaijongo Geoffrey, baba wa mkurugenzi huyo, alisema kuwa baada ya kupata taarifa mwanawe hakufika nyumbani na wala haonekani, walianza kuzunguka katika hospitali na vituo vya polisi kuulizia. Kote walipata ushirikiano mzuri.

Alimshukuru Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro kwa kuwa karibu nao katika kipindi chote cha kumtafuta ndugu yao, akieleza kuwa juzi akiwa Makumbusho, alipigiwa simu kwa namba asiyoijua, alipopokea akasikia sauti ya kijana wake.

"Kwa kweli nilishtuka sana lakini baadaye ikabidi nijipe moyo nikamwuliza ni wewe Maclean, akajibu "ni mimi baba!" Nikamuuliza 'uko wapi?' Akasema 'nipo Kigamboni Buyuni', huko nilikuwa sikufamu ndio nimefika leo (juzi). Kwa hiyo, kitu cha kwanza nilifika Central Polisi kuripoti kwamba kijana tuliyekuwa tunamtafuta amesema yuko mahali fulani.

"Nilifikiria kwamba labda ni mtego, hivyo nilitaka nipate msaada wa polisi, lakini tulikwenda kwa haraka sana bila kuchelewa, ilikuwa majira ya saa 12:30 jioni, tulitafuta eneo husika tukamkuta kijana alikuwa mdhaifu, polisi wakasema kwa utaratibu yuko mikononi mwao mpaka watakapojua yuko salama kiasi gani," alisema Geoffrey.

Kamanda Muliro alisema wanaendelea kufanya uchunguzi zaidi ili wajue ni kitu gani hasa kilichosababisha mkasa huo kutokea, akieleza kuwa wamemsikiliza sana Mwaijongo na kwamba kuna vitu fulani wanataka kuvijua.

"Jambo la kwanza tumempata, la pili tunachunguza kwamba ni kitu gani kwa sababu sijahitimisha, bado tunafuatilia. Kwa kuwa anasema alikwenda mwenyewe Kigamboni, hivyo zilizotoka ni taarifa za awali," alisema Kamanda Muliro.




Kiongozi wa kijeshi wa Guinea Kanali Mamadi Doumbouya (katikati) ambaye amejipandisha cheo kuwa Jenerali. **PICHA: MTANDAO**

# Kiongozi Guinea ajipandisha cheo kuwa jenerali

**CONAKRY,** Guinea

KIONGOZI wa kijeshi wa nchini Guinea, Kanali Mamadi Doumbouya amejipandisha cheo na kuanzia sasa anatambulika kama jenerali wa jeshi katika taifa hilo lenye mgogoro wa kisiasa.

Kanali Doumbouya alitangaza uamuzi huo juzi wakati nchi hiyo ya Afrika Magharibi iliyokabiliwa na mapinduzi ikiashiria hatua za kuimarisha zaidi mamlaka ya vikosi vya kijeshi ambavyo tayari vina nguvu.

Ilielezwa kuwa kiongozi huyo wa kijeshi Januari mwaka huu pia alijipandisha cheo hadi Kanali huku akiweka wazi kuwa serikali yake ya kijeshi haitatimiza ahadi yake ya kurudisha mamlaka kwa raia watakaochaguliwa ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Doumbouya, aliingia madarakani kwa nguvu Septemba 2021 kwa kumpindua aliyekuwa Rais wa nchi hiyo Alpha Conde, ambaye alikuwa amempa cheo cha kanali mkuu wa kikosi maalum cha kijeshi kilichopewa jukumu la kumlinda mkuu huyo wa nchi dhidi ya mapinduzi ya aina hiyo.

Katika amri iliyotangazwa juzi jioni, Doumbouya ambaye wafuasi wake wamekuwa wakimsihi agombee urais baada ya serikali ya kijeshi itakapoacha hatamu alitunukiwa tuzo ya juu ya Kitaifa ya Colratier, ambayo ni ya daraja la juu kabisa nchini humo.

Ilielezwa kuwa heshima hiyo ni kutokana na juhudi zake za mara kwa mara za kukuza mshikamano wa kijamii na ushirikiano miongoni mwa watu wa Guinea.

Pia ilielezwa kuwa Doumbouya aliyejipa madaraka mapya ya Jenerali Mkuu ni mmoja wa maofisa kadhaa walionyakua mamlaka kwenye nchi za Afrika Magharibi tangu mwaka 2020, sawa na viongozi wenzake wa kijeshi wa Mali, Burkina Faso na Niger.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kiongozi huyo wa kijeshi wa Guinea, anaendeleza msako dhidi ya wapinzani, wakati ambao inatajwa kwamba viongozi wengi wa upinzani wamewekwa kizuizini, kufikishwa mahakamani huku baadhi yao wakilazimika kuikimbia nchi hiyo.

Katika wakati mwingine, ilielezwa kuwa serikali ya kijeshi ilipiga marufuku maandamano, na kwamba hatua za vikosi vya usalama za kuyazuia maandamano yasiyoidhinishwa zimesababisha vifo vya watu kadhaa, ikiwa ni kwa mujibu wa mashirika ya haki na kiraia.

Vile vile, ilielezwa kuwa vyama vitatu viliwekwa chini ya uangalizi na vyama vingine 53 vilifutiwa usajili wake mwezi Oktoba katika kile serikali ya kijeshi ilichokiita (opereshi ya kuisafisha nchi kisiasa).

Wizara ya mambo ya ndani ya Guinea, ilisema kwenye ripoti yake kwamba, kati ya vyama 211 vilivyosajiliwa, 53 vimefutwa, na vingine 54 vimesimamishwa kwa muda wa miezi mitatu huku 67 vikiwekwa chini ya uangalizi kwa miezi mitatu ambako vinaweza kusimamishwa au kufutwa endapo vitapatikana kuwa vimekiuka sheria za nchi. **DW**

TANGAZO

# Kusherehekea Miaka Minne ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi Madarakani: Kipindi cha Ukuaji na Mafanikio kwa PBZ

PBZ IKHLAS
PBZ BANK

Katika miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imepiga hatua kubwa, ikionyesha ukuaji wa kipekee na mafanikio makubwa tangu mwaka 2020. Hii imetokana na sera za kiuchumi zenye kuunga mkono na utawala bora wa serikali yake, ambapo benki imevuka malengo yake mara kwa mara na kuweka rekodi mpya za utendaji..

Mtaji wa PBZ umeongezeka kwa kiasi kikubwa, ukikua kutoka Tzs bilioni 109.67 hadi Tzs bilioni 232.19 kufikia Septemba 2024, ongezeko la kuvutia la 111.7%. Ukuaji huu wa mtaji unaonesha mazingira chanya yaliyoundwa na serikali ya Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, ambayo yameiwezesha benki kuwekeza katika mustakabali wake na kuunga mkono malengo mapana ya serikali kwa maendeleo ya kiuchumi.

Jumla ya mali za benki imeongezeka kwa kiwango kikubwa, kutoka Tzs bilioni 752.83 mwaka 2020 hadi Tzs trilioni 2.43 kufikia Septemba 2024, ambayo ni ongezeko la 223%. Ongezeko hili linaonesha jinsi sera za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, zimechangia kukuza uchumi na kutoa fursa kwa PBZ kutanua wigo wa utoaji huduma zake, kuboresha huduma zake, na kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wake.

Amana za PBZ zimeongezeka kwa kiwango kikubwa, kutoka Tzs bilioni 578.36 mwaka 2020 hadi Tzs trilioni 1.99 mwaka 2024, ongezeko la 244%. Ukuaji huu unaonesha imani kubwa ambayo wateja wetu wanayo kwa benki, ambayo imewezekana kutokana na mazingira thabiti na yenye kuunga mkono yaliyoletwa na uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt Hussein Ali Mwinyi



***Mkurugenzi Mtendaji, Arafat Haji***

Kwa upande wa faida ya PBZ kabla ya kodi ilikuwa Tzs bilioni 18.36 mwaka 2020. Kwa msaada wa sera nzuri za serikali ya Dkt Hussein Ali Mwinyi, tuna imani kwamba tutafunga mwaka 2024 na faida kabla ya kodi ya Tzs bilioni 95.94, ongezeko la zaidi ya 422%. Hii inaonesha kuwa PBZ haijanufaika tu na mazingira mazuri, bali pia imechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi.

Mtandao wa benki umekua kwa kiwango kikubwa. Mwaka 2020, PBZ ilikuwa na matawi na vituo vya huduma 23, yakiwa manne pekee kwa Uapnde wa Tanzania Bara. Kufikia Septemba 2024, tumekuwa na matawi 44, yakiwa 15 Tanzania Bara, na tunapanga kufungua mengine mawili kwa upande wa Bara na moja Zanzibar kabla ya mwisho wa mwaka. Utanuzi huu hauishii kwenye matawi pekee, kwani PBZ imeongeza mtandao wake wa mawakala kutoka 86 mwaka 2020 hadi zaidi ya 1,350 sasa. Pia, tumezingatia maendeleo ya kidijitali kwa kuboresha mfumo elekezi (Mobile App) kupitia simu janja na kutanua mtandao wa ATM, sasa tukitoa huduma kupitia zaidi ya ATM 960 kote Tanzania, kuhakikisha huduma za kifedha zinapatikana kwa kila mtu.

Kitabu cha mikopo cha PBZ pia kimekua kutoka Tzs bilioni 469.71 mwaka 2020 hadi Tzs trilioni 1.23 kufikia Septemba 2024, ongezeko la 162%. Ukuaji huu unaonesha kuwa watu na biashara nyingi zaidi wanapata ufadhili wanaohitaji, jambo linalosaidia kuchochea shughuli za kiuchumi na maendeleo nchini Tanzania.

Kwa mafanikio haya, PBZ inajikuta ikihitaji kurudi kwenye meza ya kupanga mikakati ili kuunda mpango mpya. Mpango wetu wa sasa umefikia malengo yake mengi, na sio tu kuyafikia bali kuyavuka kwa kiwango kikubwa. Huu ni uthibitisho wa mafanikio makubwa ya benki katika kipindi cha miaka minne iliyopita, yaliyowezeshwa na hali thabiti ya kiuchumi na uongozi wenye busara wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Ukuaji wa PBZ unaonesha dhamira ya benki ya kuunga mkono malengo ya kiuchumi ya serikali, kukuza ujumuishaji wa kifedha, na kuendeleza maendeleo ya kiuchumi kote Tanzania. Tuna matumaini ya kuendelea na safari hii chini ya uongozi bora wa Mheshimiwa Rais, tukikumbatia fursa mpya za kuhudumia watu wetu na kuweka malengo makubwa zaidi kwa siku zijazo.






# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVER KUBORESHA KIKOSI

LIVERPOOL wana malengo ya kuboresha kikosi chao Januari na wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 24, kutoka Real Madrid. (***Team talk***)

### JESUS ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inataka kumsajili mshambuliaji wa Botafogo ya Brazil, Igor Jesus mwenye umri wa miaka 23, kwa mkataba pauni milioni 30. (***Sun***)

### UNITED NA DAMU CHANGA

MANCHESTER United inataka kununua damu changa ili kumkuza na kuwa nyota katika klabu hiyo, na wanaamini kuwa mchezaji mmoja ambaye angefaa ni kiungo wa kati wa England, Chris Rigg mwenye umri wa miaka 17, ambaye thamani ya Sunderland ni pauni milioni 20 hadi 30. (***Football Insider***)

### OSIMHEN KUBAKI GALATASARAY

KLABU ya Galatasaray sasa inatumai kumsajili mchezaji anayelengwa na Chelsea, Victor Osimhen kwa mkataba wa kudumu, wakiwa tayari wamemchukua kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Napoli, huku klabu hiyo ya Uturuki ikiwa tayari kulipa euro milioni 50 kwa mshambuliaji huyo wa Nigeria. (***Sozcu***)

### LOOKMAN AFUATILIWA

KLABU ya West Ham imejiunga na klabu kadhaa zinazomfuatilia winga wa Atalanta na Nigeria, Ademola Lookman, 27. (Teamtalk)

### ADEYEMI AWANIWA

CHELSEA inatazamia kutaka kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akilengwa na Liverpool. (***Football Insider***)

### ALONSO NA REAL MADRID

MATARAJIO ya kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso na winga wao wa miaka 21 wa Ujerumani, Florian Wirtz wote kujiunga na Real Madrid yanazidi kuwa ya kweli. (***Sky Sport Germany***)

### WANAWINDWA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Brentford na Cameroon, Bryan Mbeumo mwenye umri wa miaka 25, na straika wa Bournemouth raia wa Ghana, Antoine Semenyo (24), ni miongoni mwa wachezaji wanaowindwa na Liverpool, huku mshambuliaji wa Misri Mohamed Salah mwenye miaka 32, akiwa katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake hapo Anfield. (***Sky Sports***)

### REIS ATAKIWA ARSENAL

KLABU ya Real Madrid inaweza kushindana na Arsenal na Chelsea kumsajili mlinzi wa Brazil, Vitor Reis mwenye umri wa miaka 18 kutoka Palmeiras. (***Athletic***)

### ORTEGA KWENYE RADA

MCHEZAJI wa Manchester City, Stefan Ortega, yuko kwenye rada za Bayer Leverkusen, lakini bado hawajatafuta mbinu madhubuti kwa mlinda mlango huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 31. (***Sky Sport Ujerumani***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AITOA ARSENAL MBIO ZA UBINGWA EPL

●●●Asema walistahili kupoteza dhidi ya Newcastle juzi na kwamba alichanganyikiwa kuona...

**NEWCASTLE,** England

MIKEL Arteta amekataa kuhusishwa na nafasi ya Arsenal ya kutwaa ubingwa baada ya timu yake kupokea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Newcastle United Jumamosi.

Bao la kichwa la Alexander Isak dakika ya 12 lilimaliza mpambano mkali katika Uwanja wa St James' Park, ambapo Arsenal walisajili shuti moja pekee lililolenga lango.

Arsenal sasa wako pointi saba nyuma ya vinara, Liverpool baada ya ushindi wao dhidi ya Brighton baadaye Jumamosi, na Arteta alisema: „Ninaelewa hilo, lakini baada ya mechi nane, tisa au 10 mwaka jana hatukuzungumza kuhusu ubingwa.

**"Ni kuhusu jinsi unavyoitikia hilo. Hatutapata maneno au majibu sahihi kueleza jinsi tunavyohisi. Tunapaswa kuiweka kwenye uwanja huo Jumatano usiku dhidi ya Inter Milan katika Ligi ya Mabingwa Ulaya."**

Arteta alipendekeza Newcastle ifanye mchezo huo kuwa wa kimwili zaidi baada ya bao la Isak na anaamini timu yake ilipaswa kukabiliana na kazi hiyo vema zaidi.

"Tulistahili kupoteza leo (juzi)," alisema.

"Nilidhani tulianza vizuri na tulikuwa na uwezo mkubwa. Hatukulinda boksi vya kutosha, sifa kwao. Walifunga bao zuri kwa mpira mzuri.

"Halafu mchezo unabadilika na unaanza kucheza mchezo tofauti. Unapaswa kuzoea na hatukufanya vizuri vya kutosha. Nimechanganyikiwa sana.

"Tuliburuzwa kwenye mchezo ambao wanautafuta kila mara na hatukuweza kucheza mchezo ambao tulitaka."

# GUARDIOLA: MAJERUHI SI KISINGIZIO CHA KUFUNGWA



**LONDON,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema majeruhi hayawezi kuwa kisingizio cha wao kufungwa mabao 2-1 na Bournemouth kwenye mechi ya Ligi Kuu England Jumamosi.

Kipigo hicho kiliishusha City hadi nafasi ya pili, pointi mbili nyuma ya Liverpool, ambao walishinda mabao 2-1 dhidi ya Brighton & Hove Albion katika mchezo wa mapema.

"Sijui nini kimetokea. Ningependa kuwaambia kama wachezaji hawa hawakuwa majeruhi, tungeshinda, lakini hakuna anayejua," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Vijana wanatoa kila kitu, lakini haitoshi kushindana dhidi ya timu hiyo wakati huo."

Kupoteza kwa City kulikuja kutokana na kichapo cha katikati ya wiki kutoka kwa Tottenham Hotspur katika Kombe la Ligi raundi ya nne.

Guardiola alisema timu yake ililipa gharama kwa kukosa umakini huku Bournemouth ikishinda kupitia mabao ya Antoine Semenyo na Evanilson.

"Hatukuweza kuendana na kiwango," alisema. „Hali zote na mipira mirefu, hatukuweza kushinda.

"Na usiposhinda mipira ya aina hii kwa Semenyo na wengine, mabeki wetu wa kati na washambuliaji wanapaswa kujilinda zaidi.

"Tuna wachezaji wenye ufiti na wengine hawana kwa sababu hatukuweza kufanya mazoezi kutokana na majeraha. Lakini tulijua."

Ijumaa Guardiola alisema amewataka nyota wake kucheza kwa umakini na anahofia kuwa anaweza kuwa na wachezaji 11 tu wanaofaa kushiriki mechi dhidi ya Bournemouth.

City tayari walikuwa wamewakosa Jack Grealish, Rodri na Oscar Bobb na katika mahojiano yake kabla ya mchezo, Guardiola alisema Ruben Dias na John Stones pia watakuwa nje kwa muda mrefu kidogo.

Nahodha Kyle Walker alikuwa mmoja wa wachezaji kadhaa ambao hawakutarajiwa kucheza Jumamosi, lakini alianza, huku Kevin De Bruyne akirejea kwenye benchi baada ya kukaa nje kwa muda mrefu kutokana na jeraha.

"Kyle katika muda wa siku 16 hakufanya mazoezi nasi, alifanya juhudi kubwa," alisema Guardiola.


"Labda ni bora, lakini hatuko katika nafasi hiyo," alisema. „Hatutumii hilo kama kisingizio, lazima utoe sifa kamili kwa Bournemouth."

City wana muda mchache wa kupona huku wakielekea Lisbon kucheza na Sporting kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kesho, Jumanne.

"Ni ratiba ambayo tumeshughulikiwa, hakuna visingizio," aliongeza.

Ushindi wa Bournemouth ulikuwa wa kwanza kwao dhidi ya City katika historia ya klabu hiyo na mashabiki wa ‚Cherries' kwenye Uwanja wa Vitality waliimba kwa shangwe: „Je, tunaweza kucheza nawe kila wiki?"

# Flick apuuzia ubingwa Barca



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, alipuuzilia mbali wazo kwamba timu yake imechukua nafasi ya Real Madrid na kuwa ndiyo inayopewa nafasi kubwa ya kushinda ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya ushindi wa mabao 4-0 wa Clasico wikendi iliyopita.

Ushindi wa Barca dhidi ya Madrid katika Uwanja wa Bernabeu, ukiwa ni mchezo wao wa 10 kati ya michezo 11 ya ligi chini ya Flick, uliwasogeza kwa pointi sita kileleni mwa msimamo.

Jana Jumapili walikuwa wakicheza na Espanyol kwenye mchezo wa dabi ya Katalunya pale katika dimba la Olympic.

"Kuna njia ndefu ya kwenda," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari.

"Mambo mengi yanaweza kutokea ambayo hatuyatarajii, tuko katika hali nzuri na tuna mtiririko, lazima tuendelee. Huu ni mpango wetu. Ni kama tunafanya kila wakati, tunajiandaa vema kwa mechi ijayo.

"Tunaposhinda, ni vema pia kusherehekea hili, lakini lazima tuzingatie mechi inayofuata. Ni safari ndefu hadi mwisho wa ligi."

Oktoba, Flick alimaliza kwa rekodi ya ushindi wa asilimia 100 katika mashindano yote, ambayo ilimfanya kuwa kocha Bora wa Mwezi wa LaLiga.

Frenkie de Jong, Dani Olmo na Gavi, ambao wote waliingia wakitokea benchi katika ushindi dhidi ya Madrid, wote sasa wapo fiti baada ya kurejea kutoka kuuguza majeraha ya muda mrefu.

## Slot azidi kung'ara akiwa na Liverpool

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot, alimsifu Mohamed Salah wakati bao la fowadi huyo wa Misri lilipoifanya timu yake kutoka nyuma na kuwalaza Brighton & Hove Albion mabao 2-1 na kwenda kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

Salah aliihakikishia Liverpool pointi tatu katika Uwanja wa Anfield na kuifanya timu ya Arne Slot kuwa pointi mbili zaidi ya mabingwa waliokumbwa na majeraha Manchester City ambao walipoteza katika ligi kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miezi 11, baada ya kuchapwa 2-1 na Bournemouth.

Kukamilisha siku ya ndoto kwa Liverpool, wapinzani wenzao wa ubingwa Arsenal walifungwa bao 1-0 na Newcastle United.

Liverpool walirudi nyuma baada ya dakika 14 dhidi ya Brighton huku mchezaji wa Kimataifa wa Uturuki, Ferdi Kadioglu, akiruka katika juhudi za kushangaza huku wageni wakichukua udhibiti.

"Bao la pili lilikuwa maalum la Mo Salah," alisema Slot BBC Sport.

"Si mara ya kwanza na si mara ya mwisho kufunga kutoka nafasi hiyo."

Slot amefurahia mwanzo mzuri zaidi wa kocha yeyote mpya wa Liverpool tangu achukue nafasi ya Jurgen Klopp na ushindi wa Jumamosi ulikuwa wa 13 kwa timu yake katika mechi 15 kwenye mashindano yote.

Ushindi mara nane kwa Slot katika mechi zake 10 za kwanza za Ligi Kuu England pia ni mwingi kuwahi kupata kocha wa Liverpool katika mechi zake 10 za kwanza za Ligi Kuu akiwa kocha.

Ingawa vipigo vya City na Arsenal vilikuwa bonasi, Mholanzi huyo alisema anajali tu upande wake.

"Si kwa sababu ya matokeo hayo, lakini ninahisi maalum kwa sababu tulikabiliana na Arsenal wiki iliyopita ambao ni timu ngumu sana," alisema.

"Leo (juzi), tulikabiliana na ubora na wazo lile lile kuhusu soka na mara zote mbili tulilazimika kutoka nyuma ili kupata matokeo. Hilo ndilo linalonifanya kuwa siku yangu, si matokeo ya michezo mingine."

Jambo moja hasi siku hiyo lilikuwa ni beki wa kati Ibrahima Konate aliyetoka wakati wa mapumziko akiwa na jeraha la mkono.



## HABARI MICHEZO

### *Gamondi aukubali muziki wa Azam FC*

INATOKA UKURASA 24

Pamoja na kupoteza, bado Yanga ipo kileleni ikiwa na pointi 24 kwa mechi tisa ilizocheza, Singida Black Stars ikirejea nafasi ya pili baada ya suluhu dhidi ya Coastal Union ikiwa na pointi 23 kwa michezo 10 iliyocheza, Simba ikiwa nafasi ya tatu na pointi zake 22 kwa michezo tisa iliyocheza.

Ushindi wa juzi umeifanya Azam kufikisha pointi 21 kwa michezo 10 iliyocheza ikiwa kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

### Stars yafungwa ikifuzu CHAN

INATOKA UKURASA 24

zo wa uwanjani, badala yake imefuzu kutokana na uenyeji kwani fainali hizo zitachezwa mwakani hapa nchini, Kenya na Uganda, ikiwa ni majaribio ya maandalizi ya fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027 katika nchi hizo.

Ushindi huo umeipa Sudan tiketi ya kufuzu fainali hizo, huku nchi hiyo ikiwa inacheza mechi zake za nyumbani nchini Mauritania kutokana na nchi yao kukubwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Katika mchezo wa jana, Stars ilitumia wachezaji wengi wa timu ya vijana, Ngorongoro Heroes, pamoja na wakongwe wachache akiwamo Manula ambaye ndiye nahodha wa kikosi hicho.

Ilikosa mabao maengi kupitia kwa mastraika wake, Selemani Mwalimu, Edgar William, na wengine ambao kwa kiasi kikubwa wameonekana kuwa na uchu wa mafanikio chini ya Kocha Bakari Shime.

Dakika moja kabla ya mechi kumalizika, straika Nassor Saadun, alizawadiwa kadi nyekundu baada ya kucheza rafu tatu mfululizo, moja alionywa, ya pili alipewa kadi ya njano na ya tatu nyekundu kwa dakika zisizozidi mbili mbili kila tukio.

Alikuwa ameingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Hijjah Shamte. Straika huyo wa Azam FC, alicheza mechi ya pili mfululizo baada ya jana kuwa mmoja wa wachezaji waliocheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, timu yake ikicheza dhidi ya Yanga na kushinda bao 1-0.

# SERIKALI YATAKA RIADHA KUAMKA VISIWANI Z'BAR

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema kwa sasa ni zamu ya mchezo wa riadha kuamka na kupanda juu baada ya soka.

Akizungumza kwenye mbio za nusu marathon za 'Tigo-Zantel Marathon 2024' zilizofanyika jana Zanzibar, Makamu wa Pili wa Rais Abdulla, alisema mchezo wa soka Zanzibar umepiga hatua ambapo kumekuwa na timu nyingi na vijana wengi wanashiriki, hivyo lazima na riadha nao uinuke visiwani humo.

"Nawapongeza waandaaji wa mbio hizi, ni wakati sasa kwa mchezo huu wa riadha kuinuka huku Zanzibar kama ilivyo soka," alisema.

Makamu wa Pili wa Rais alimwakilishi Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye alikuwa mgeni rasmi na kushiriki matembezi ya kilometa tano.

Mbio hizi zilizofanyika kwa msimu wa nne mfululizo, zilishirikisha mamia ya wakimbiaji kutoka Zanzibar na nje ya visiwa hivyo.

Awali, akizungumzia mbio hizo, Mkuu wa Biashara wa Tigo- Zantel, Isaack Nchunda, alisema wanaamini mbio hizo zimeongeza chachu ya ukuaji wa uchumi visiwani humo.

"Tunaamini mbio hizi zinatupa jukwaa bora zaidi la kutangaza utalii wa Zanzibar, kukuza vipaji vya wanariadha, kuimarisha afya, na kuchangia katika uchumi wa bluu visiwani hapa," alisema Nchunda.

Aidha, alisema dhamira ya kampuni hiyo ni kuendelea kuleta mabadiiko chanya kwenye jamii kwa kuwekeza katika miradi na matukio yanayogusa maisha ya wananchi.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (wa pili kulia), akishiriki mbio za Tigo-Zantel Marathon zilizofanyika jana visiwani humo. Abdulla alimwakilishi Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshindi Samia Cup Jimbo la Babu Tale alamba mamilioni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TIMU ya soka ya Matuli kutoka Kata ya Ngerengere Wilaya ya Morogoro, mkoani hapa, imejinyakulia kitita cha Sh. milioni tano baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kiroka kwenye mchezo wa fainali wa michuano ya 'Samia Cup', uliopigwa katika Tarafa ya Ngerengere juzi, Jumamosi.

Kombe hilo la Samia Cup liliaonzishwa na Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Hamis Taletale maarufu kama Babu Tale, lilihusisha timu zote kutoka kwenye Kata 14 jimboni hapo lengo likiwa ni kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha kupiga kura uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na kusaka vipaji vipya.

Mshindi wa pili ambayo ni timu ya Kiroka, ilijinyakulia Sh. milioni tatu, huku ya tatu timu ya Gwata ikizawadiwa Sh, milioni mbili wakati Kinole ikiambulia Sh. milioni moja kwa kushika nafasi ya nne katika michuano hiyo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi kombe pamoja na fedha hizo kwa washindi, Babu Tale alisema mashindano hayo yamegharimu zaidi ya Sh. milioni 45 ikijumuisha na kila timu kupewa Sh. 500,000 na jezi za kisasa jozi mbili, maandalizi ya michuano hiyo pamoja na zawadi kwa washindi na wafungaji wa 'Goli la Mama'.

"Katika mashindano haya yaliyohitimishwa leo [juzi] ya Samia Cup, yalichezwa kwenye kata zote 14 za tarafa tatu za Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki, na kila timu zilipewa jezi jozi mbili, Sh. 500,000 na mipira, na michuano hiyo ilifanyika kwa mtindo wa nyumbani na ugenini," alisema.

Hata hivyo, Babu Tale alisema malengo ya mashindano hayo yamefikiwa kama ilivyopangwa ikiwa ni pamoja na wananchi kuhamasika kwa wingi kwenda kujiandikisha, lakini pia wameibua vipaji vya zaidi ya wachezaji watano kutoka kata mbalimbali na tayari ameshawasiliana na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya kuwafanyia majaribio.

Alisema baada ya kumalizika michuano hiyo, anatarajia kuanzisha ligi nyingine itakayoanzia ngazi ya kila kijiji kilichopo kwenye Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki ili kuendelea kuibua vipaji na kuleta furaha kupitia michezo.

Akikabidhi Kombe hilo, Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Morogoro, Solomoni Kasaba, alipongeza jitihada za mbunge huyo kwa kuwaunganisha wananchi kupitia michezo.

Katibu huyo, alisema michezo hiyo ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya chama hicho na kumtaka Babu Tale kuendelea kueneza michezo katika Jimbo hilo kila wakati ili kuvumbua vipaji.

Michezo
Jumatatu Novemba 4, 2024
Nipashe



Arteta aitoa Arsenal mbio za ubingwa EPL UKURASA 21

# Stars yafungwa ikifuzu CHAN



Straika wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Selemani Mwalimu (katikati) na winga wa kushoto, Sabri Kondo (kushoto), wakisaka njia ya kumpita beki wa kati wa Sudan, Mohamed Saeed Ahmed, katika mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ligi za Ndani (CHAN), uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana, ikishuhudiwa Stars ikifungwa kwa mikwaju ya penalti 6-5, baada ya matokeo ya jumla kuwa 1-1 katika michezo yote miwili nyumbani na ugenini. Timu zote zimefuzu, Sudan ikifuzu kwa ushindi huo na Stars kama wenyeji wa fainali hizo zitakazofanyika Tanzania, Kenya na Uganda hapo mwakani. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars imefungwa kwa mikwaju ya penalti 6-5 na Sudan katika mchezo wa kusaka tiketi ya kufuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana.

Timu hizo zililazimika kupigiana penalti baada ya matokeo ya jumla kuwa bao 1-1 kwa michezo yote miwili, Sudan ikishinda bao 1-0 kwenye mchezo wa kwanza uliopigwa nchini Mauritania, kabla ya jana Stars nayo kushinda 1-0, lililowekwa ndani ya wavu na Crispian Ngushi dakika ya 32.

Penalti za Sudan zilifungwa na Walieldin Khidir, Mohamed Abdulrahman, Salaheldin Adil, Ramadan Agab na Ally Abdallah, huku za Stars zikizamishwa kimyani na Shekhan Ibrahim, Daud Brayson, Abdallah Said, Sabri Kondo na Abdulkarim Kassim, huku Paul Peter mkwaju wake ukipanguliwa na golikipa Ahmed El Fatih.

Nahodha wa Stars, Aishi Manula, ambaye mashabiki walikuwa na matumaini makubwa ya kumuona akiokoa penalti kama ilivyo sifa yake, lakini zote zilitinga wavuni.

Matokeo hayo yanaifanya Stars kushindwa kufuzu fainali za CHAN kwa uwe-

INAENDELEA UKURASA 23

# GAMONDI AUKUBALI MUZIKI WA AZAM FC

## ●●● Sasa asema hakuna timu isiyofungwa, awaomba radhi mashabiki huku akitaja sababu ya kipigo...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amewataka wanachama na mashabiki kuangalia mbele, na kukubali kuwa wamepoteza mchezo wao dhidi ya Azam kwani hakuna timu yoyote duniani ambayo haifungwi.

**Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo na Azam FC, ikichapwa bao 1-0, lililowekwa ndani ya wavu na Gibril Sillah, kocha huyo alisema hakuna yeyote anayependa kupoteza mechi, lakini ni lazima kuukubali ukweli.**

Yanga imepoteza kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya kucheza michezo minane ikishinda yote na kutoruhusu wavu wake kuguswa, lakini rekodi zote mbili zimevunjwa kwa wakati mmoja juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

"Hakuna anayependa kupoteza, lakini inabidi tukubali, nawapa pole sana na samahani mashabiki wa Yanga, wajue huu ni mpira na siku moja timu itapoteza mechi, lazima waamini hivyo, hakuna timu yoyote duniani ambayo haipotezi," alisema.

Hata hivyo, Gamondi alisema kilichoigharimu timu yake ni kadi nyekundu aliyopewa beki wake, Ibrahim Hamad 'Bacca' kuwa iliwaathiri kwa kiasi kikubwa na kuisababisha kupoteza mchezo huo.

"Kilichotugharimu ni kadi nyekundu, kama tungekuwa sawa na wachezaji wa Azam, ingekuwa mechi nzuri zaidi. Nimemshangaa mwamuzi kwa sababu ametoa kadi nyekundu wakati tukio kama hili lilitokea katika mchezo wetu dhidi ya Simba, lakini kadi nyekundu haikutoka.

"Nilichofurahi ni kwamba pamoja na kucheza pungufu tumetengeneza nafasi nyingi, na hasa kipindi cha pili pamoja na muda wote tulicheza vizuri kuliko Azam, tukatengeneza nafasi mbili za wazi, walikuwa na bahati," alisema Gamondi.

Aliwapongeza Azam na kocha wao, Rachid Taousi, aliyesema ni rafiki yake mkubwa, wakifahamiana kwa miaka 25 wakiwa wameshawahi kufanya kazi pamoja, akiahidi watarejea wakiwa imara zaidi katika michezo inayofuata.

Kocha wa Azam, Taousi, alionesha furaha yake kwa kuifunga Yanga, akiwa kocha wa kwanza kufanya hivyo kwenye Ligi Kuu, huku pia timu yake kuwa ya kwanza kuondoa ubabe wa timu hiyo msimu huu.

"Tumekuwa timu ya kwanza msimu huu kuifunga Yanga, tumekuwa wa kwanza kufunga bao dhidi yao, na mimi nimekuwa kocha wa kwanza kumaliza ubabe wao, ushindi huu naupeleka kwa mashabiki wa Azam na mabosi wa klabu.

"Haikuwa rahisi, tumecheza na timu kubwa na wachezaji bora wenye viwango vya juu, tuliingia na mipango yetu ambayo imetusaidia sana," alisema kocha huyo ambaye naye akikiri kwamba wanafahamiana vizuri na Gamondi kwa miaka mingi, wanajuana na ni rafiki yake mkubwa.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >